

KUIKUBALI NJIA YA

MUNGU ILIYOWEKWA

KATIKA WAKATI WA MWISHO



[Ndugu Carl Williams anasema, “Unaendeleaje, Ndugu Branham?”—Mh.] U hali gani, Ndugu Carl? Njema. Asante. [Ndugu Williams anazungumza na kusanyiko, “Ketini, tafadhali.”] Sogeza kiti kingine nyuma. Vema. Ni changu? [“Naam.”] Hum! Hiki hapa.

² Vema, hakika ni vema kurudi nyumbani mwa Bwana, usiku wa leo, na hasa sana hii, kwa sababu nilikuwa na majaliwa ya kuiweka wakfu nyumba hii ya Bwana, wakati fulani uliopita, wakati Ndugu yetu wa thamani Sharrit alipopajenga mahali hapa, nasi tuliweka wakfu kwa Bwana kwa ajili ya utumishi Wake. Na ni vema kuwa nyumbani mwa Mungu wakati wowote, siyo? Ni mahali pazuri kweli kuwapo.

³ Na huku chini kwenye ukanda huu wa baridi, ambako ni . . . Nilikuja huku chini nipate kuitoroka hali ya baridi, ndipo nikainga moja kwa moja ndani yake. Nilisema jana usiku, “Natumaini sikuwaletae nyinyi nyote matatizo haya yote.” Vema, mwajua, wanasema msimu wa kiangazi hutumia likizo yake ya baridi kali huku. Na labda baridi kali imekuja kuichungulia, kuona jinsi ilivyokuwa inaendelea. Lakini ni vyema ku—kuwa hapa wakati wowote.

⁴ Daima nimekuwa na u—uvutio wa Phoenix, tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Napenda Phoenix. Na Phoenix palikuwa ndipo mahali pangu pa kwanza kuwahubiria watu wasiokuwa jamii ya wazungu. Hao walikuwa ni Wahindi. Nilipanda nikaenda mahali walipotengewa. Nadhani huenda kukawa na watu hapa usiku wa leo wanaokumbuka wakati nilipomtolea Mungu ahadi jukwaani: kama angemponya mlevi sugu na mwanamke mwenye TB, ningenda kwenye hifadhi ku—kuwahudumia Wahindi. Nao wakanikumbusha juu yake. Nao wote wawili waliponywa. Basi nikaenda kwenye Hifadhi ya Apache, na huko Bwana akatupa ushindi mkuu.

⁵ Siwezi kulikumbuka jina la mama huyo aliyeponywa kansa huko juu. Kilikuwa ni kisa cha ajabu sana. Ninaamini alikuwa ni mmishenari kule juu, Assemblies of God, kama ninavyokumbuka. Tuliambatana naye, Mitchell. Na hiyo ni kweli. Kuna mtu yeyote hapa aliyekuwako kwenye mkutano huo

huko juu kwenye hifadhi basi, usiku huo? Nilifikiri... Naam. Hiyo ni kweli.

⁶ Ni—nilidhani nilikuwa nikikabiliana nalo. Ni—nisingeweza kuwafanya waelewe nilichokuwa nikimaanisha. Kamwe sitausahau usiku huo. Kulikuwako na... kitambo kirefu baada ya mimi kuhubiri muda fulani, na kuwaambia habari za Kristo. Nilikuwa nimesimama kwenye vipandio vya ukumbi wa hiyo misheni. Nao walikuwa wamepajaza mahali hapo kabisa, halafu wote walikuwa nje. Kwa hiyo nilikuwa nikiwazungumzia. Basi jambo moja kuu mno, usiku huo, lilikuwa ni yu—yule ndugu mzee wa Kihindi waliyekuwa wamemleta juu ya ubao, na mapema wakati fulani karibu mapambazuko. Na wao—wao walikuwa wamelowa maji, ambapo walikuwa wamevuka m—mto. Wakauvukia kule chini, mahali fulani, wakamwingiza ndani.

⁷ Nikamuuliza jamaa huyo mdogo. Nikasema, “Hivi huogopi utashikwa na nimonia?”

Akasema, “Yesu Kristo ananilinda. Namleta baba yangu.”

“Vema.” Nikasema, “Unaamini ataponywa?”

“Naam.”

⁸ Alikuwa akitetemeka kwa kupooza. Hao wavulana wawili wadogo walikuwa wamembeba. Nikamwomba huyo mzee.

⁹ Baada ya kitambo kidogo nikasikia kitu fulani kikipiga mayowe. Nikatazama chini; mzee huyo alikuwa ameubeba ule ubao mwenyewe mgongoni mwake, anazunguka, akimpungia kila mtu mkono. Imani rahisi tu kuamini, ndiyo tu inayohitajika.

¹⁰ Ninakumbuka usiku huo, maskini mwanamke mzuri wa Kihindi, alikuwa na misuko mirefu ya nywele iliyoning’inia chini. Naye alikuwa kwenye mikongojo, nayo ilikuwa kabisa ni ya kujitengenezea nyumbani, hiyo, ni kama vijiti vya kifagio chenye kipande cha ubao juu yake, kama mbili kwa nne, kisha kinazungushiwa matambara. Na, kwa kweli, aliyefuata alikuwa... Alikuwa kwenye mstari, uliotoka ndani ya hilo jengo. Lakini kulikuwako na maskini mvulana mdogo, wa Kihindi, jamaa mdogo aliyeonekana mwenye nguvu sana. Aliwatangulia hao wote kuingia, apate kuwa mstarini. Naye maskini bikizee huyo alikuwa akijaribu kuitoa fimbo yake. Basi alikuwa ameona visa viwili ama vitatu vya uponyaji kabla hajaingia mstarini.

¹¹ Nami nikawaza, hapo aliponiangalia, na hayo makunyanzi makubwa mno, yenye kilindi, na machozi yakikatia kwenye mitaro hiyo mashavuni mwake, nikawaza, “Mama wa mtu fulani.” Kamwe sikusema neno moja kwake, sikumwomba, chochote kile. Yeye aliinua tu macho akanitazama. Na wakati akifanya hivyo, alinikabidhi tu hiyo mikongojo akaenda zake, rahisi tu hivyo.

¹² Mwanangu anajaribu kunirekebisha hapa. Mnaweza kusikia vizuri hivyo? Nilisoma hadithi fulani leo kuhusu ngu—ngu—nguruwe akipelekwa madhabahuni, nami nadhani mliona. [Mtu fulani anarekebisha maikrofoni ya Ndugu Branham—Mh.] Sasa, hilo linasikika bora zaidi, kwa vyovyote vile. Hivyo ndivyo maisha yanavyoenenda. Yana vifundo vingi sana ndani yake kwa vyovyote vile, sivyo?

¹³ Sasa watu wamesimama, na—nasi ha—hatutaki kuchukua wakati mwingi zaidi kuliko tuwezao kumudu. Nanyi ni watu wazuri sana, mpaka ni—ningetaka tu kuwazungumzia kwa muda mrefu.

¹⁴ Basi tupo hapa sasa kuutembelea Ushirika wa Wafanyabiashara wa Full Gospel. Na mkutano wa kwanza unafanyiwa huko Ramada, kuanzia sehemu ya mwisho ya... Hebu tuone, ni tarehe ngapi? [Mtu fulani anasema, "Ishirini na nne."—Mh.] Ishirini na nne. Ishirini na nne hadi ishirini na nane, katika Hoteli ya Ramada. Na kutakuwako na wahubiri wazuri sana kule, Ndugu Oral Roberts na wengine wengi. Nami... Daima tunakuwa na wakati mzuri. Ambapo, watu wanapokusanyika pamoja namna hiyo, tunakuwa na wakati mzuri sana kwenye Hoteli hii ya Ramada.

¹⁵ Huenda ikawa mimi na Ndugu Oral tutafanya ibada ya uponyaji kule. Huwezi kujua. Hilo lingekuwa ni jema tu. Naam. Kwa hiyo—kwa hiyo sisi—kamwe hatujawahi kuwa na mmoja pamoja. Sijui vile angewazia kuhusu kuwa na mmoja, mimi na yeye pamoja, lakini niko tayari. Kama anaweza kunivumilia, mbona, tutajaribu, halafu tuwaombe wagonjwa.

¹⁶ Nasi hatujakuwa tukifanya ibada za uponyaji, ikiwa mmeona. Hatujakuwa tukisambaza kadi za maombi wala chochote kile, kwa sababu ya msongamano wa hayo makanisa madogo, mwajua. Nao watu, ni vigumu kuwaingiza na kuwatoa watu. Halafu basi unapofanya hivyo, inasababisha msongamano wa kuchanganyana huko, naye mkuu wa zimamoto asingalifurahia hilo. Kwa hiyo kwa namna fulani tuliachana tu na ibada za uponyaji kufikia sasa mikutanoni, nasi tumekuwa tu tukijaribu kuleta Ujumbe mdogo, rahisi wa Injili. Kuninii... Nao uwepo wenu, na ushirikiano pamoja nami, na maombi yenu kwa ajili yangu, hunitia moyo kuwa hapa. Nami ninatumaini jumbe hizi ndogo zinawatia moyo kuendelea, mkimwishia Kristo.

¹⁷ Nami nimeona, mara nyingi, watu wanatoka kanisa moja wanaingia lingine. Na hilo linatufanya sisi sote kufahamiana, na—na tunakuwa tu... kupendana sana mmoja kwa mwingine. Ninapenda hilo. Ni afadhali basi tuketi pamoja hapa, mahali pa Mbinguni, maana tunaenda mahali kama hapo ambapo tutakuwa pamoja katika mahali pa Mbinguni, huko Mbinguni.

¹⁸ Kulikuwa na mstari mdogo wa ukosoaji niliopata hivi majuzi kwenye barua. Huenda niuelezee wakati kwa namna fulani tukiziandaa hisia zenu. Mhudumu yeyote anajua, huna budi kusema kitu kimoja ama kingine, kwa namna fulani kujiweka sawa na kusanyiko, nalo kusanyiko liwe sawa nawe. Kulikuwako na . . .

¹⁹ Wafanyabiashara waliandika makala hayo kwenye ninii yao... *Sauti* ya Wafanyabiashara, ku—kuhusu maskini... Nafikiri tutaliita tu ono. Nalo lilikuwa kidogo ni tofauti, kwa kawaida, na maono mengine niliyo nayo. Nilikuwa . . . nilikuwa nimehamishwa kutoka mahali nilipokuwa, nikatwaliwa juu. Tazameni, haikuonekana kwangu juu zaidi ya paa la jengo lile. Basi hapo mimi nilikuwa katika mahali pengine ambako niliwaona wote waliokwisha kuaga. Wengi wenu mlisoma makala hiyo, hakika. Basi mle ndani, baada ya Yeye kuniambia hao walikuwa . . . kwamba walikuwa ni nani, nao wote walikuwa ni vijana tena. Nao walikuwa ninii sana . . .

²⁰ Daima niliogopa kufa. Sio kuogopa kwamba nitapotea, bali sikutaka kuwa roho. Ninaninii tu . . . Nataka kuwa mwanadamu, mtu. Hakika, sikuzote nilifahamu kama mwanadamu, kuwapa watu mikono. Ningewazia, “Vipi kama ningefika kule nami ningekutana na Ndugu Rose, naye angekuwa ni maskini wingu jeupe, ama kitu fulani? Ninajua ilikuwa ni Ndugu Rose, kwa hisia nyingine, bali nisingeweza kumsalimia kwa mkono. Nisingeweza kuzungumza naye. Ama . . .” Ni—ningeshangaa, “Hilo si lingekuwa ni baya sana?” Lakini, nikawazia, “Halafu nitakaporudi, hakika, nitakuwa na ufufuo.”

²¹ Andiko hilo kamwe halikuwa limenijia hapo kabla, kwamba, “Maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo nyingine tayari inayongojea.”

²² Kwa hiyo asubuhi hiyo, nilikuwa nimeamka. Nilikuwa nikiwazia, “Jamani, wewe una umri wa miaka hamsini. Kama utamfanyia Bwana lolote, afadhali uharakishe. Utakuwa umezeeka kupita kiasi, baada ya kitambo kidogo.”

²³ Ndipo mara ghafla, nikanyakuliwa nikapelekwa mahali hapa, nami ningeweza kuangalia nyuma na kujiona mwenyewe hapa chini. Kamwe sijakuwa na tukio hilo. Mara nyingi nimepata maono ya kujiona mwenyewe nimesimama mahali fulani, halafu basi . . . Loo, ikiwa hulelewi, ungewazia ulikuwa umerukwa na akili. Wewe—wewe upo *hapa*, ukijiangalia mwenyewe *pale*. Na halafu unaondoka *hapa*, nawe uko ndani yako mwenyewe *pale*. Uh-huh. Huenda ikawa ni huko nyuma kabisa, miaka kadhaa mbele, na kadhalika. Ni vigumu kueleza, usingeweza, huwezi kulieleza.

²⁴ Huwezi kumwelezea Mungu. Inakubidi kumwamini. Unaona? Kama unaweza kulieleza, basi siyo imani tena. Inakubidi tu kuliadini.

²⁵ Basi baada ya Yeye kuniambia, huku nikiwaona watu hawa wote, nao walikuwa...Walikuwa na miili. Wao...Kusingeweza kuwa na dhambi. Hao wanaume na wanawake...Hao wanawake walikuwa wakinikumbatia, nao walikuwa ni wanawake. Lakini hakukuwapo na uwezekano wa kuwapo na dhambi tena, kwa sababu, mnaona, tezi za miili yetu zitabadilishwa kule. Tuna...Sisi ni jinsia mbalimbali sasa, kwa sababu hizo ni za kuuzalia ulimwengu, na ninii yetu—na ndoa yetu kuwaleta watoto. Lakini wakati huo hakutakuwapo na haja ya hilo tena. Hakutakuwapo na watoto zaidi watakaozaliwa. Hatutakuwa na tezi za jinsia katika ulimwengu mpya, mnaona, hata kidogo. Lakini, hata hivyo, mwanamke atakuwa ni mwanamke, katika umbo. Na vivyo hivyo wanaume watakuwa ni wanaume. Lakini hakutakuwapo na wa kiume na wa kike miongoni mwao, katika njia hiyo. Wala tezi hizo hazitakuwamo mle ndani, kwa hiyo hakutakuwa na njia hata kidogo kwa Shetani kuwafanyia ujanja mwingine.

²⁶ Kwa hiyo, katika hilo nikaona wanawake hawa walikimbia na kunikumbatia mimi, na kusema, “Ndugu yetu wa thamani, nina furaha sana kwamba wewe upo hapa.” Sasa, lilikuwa la kushangaza. Wote, vijana, wote ni wanawake walio warembo kabisa, nywele ndefu, mavazi marefu, mwajua, kama majoho, majoho meupe kama ya hariri. Na jinsi walivyoonekana warembo!

²⁷ Kisha hawa hapa ndugu wanakuja, ninii tu...Na wanaume wenye sura nzuri kuliko wote niliowahi kuona, wote walionekana kana kwamba wana umri wa miaka ishirini hivi. Nayo macho yao, yanang’aa. Wao, loo, walikuwa ni wanaume kwa kila wakia. Nami nikashangaa. Nao walikuwa wakininyanyua juu na kunikumbatia na kusema, “Ndugu yetu wa thamani.”

²⁸ Nilishangaa jinsi gani...Niliangalia nyuma chini na ningeweza kujiona mwenyewe *hapa* chini, bado, nimelala chini. Vema, sasa, nikawaza, “Ajabu hii.” Kisha nikauliza.

²⁹ Palikuwapo na mama wa kupendeza sana aliyejitokeza, akanikumbatia, kasema, “Loo, Ndugu Branham, tunashukuru sana wewe upo hapa, ndugu yetu wa thamani.”

³⁰ Nikamwangalia, wakati akiondoka. Ndipo Sauti hiyo iliyokuwa ikizungumza na mimi, ikasema, “Hivi humtambui huyo?”

Nikasema, “Si—simtambui.”

Akasema, “Alikuwa amepitisha miaka tisini wakati ulipomwongoza kwa Kristo.”

³¹ Naye huyo hapo, kitu kirembo sana nilichokuwa nimeona, kwa njia ya mwanamke. Nami nikasema, “Si ajabu yeye alisema

‘Ndugu wa thamani.’” Mnaona? Sasa hawezi kubadilika zaidi. Yuko hivyo Milele.

Nikasema, “Ninataka kumwona Yesu.”

³² Kasema, “Yeye yuko juu zaidi ya hapa. Siku moja Yeye atakuja, nawe utahukumiwa kwa Injili uliyohubiri, maana ulikuwa kiongozi.”

Nikasema, “Vema, hivi itambidi Paulo kuhukumiwa na umati wake?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Nilihubiri Injili ile ile aliyoihubiri. Vile vile tu hasa alivyolisema, hivyo ndivyo nilivyolisema.”

³³ Ndipo hayo mamilioni ya sauti yakasema kwa sauti kuu, “Tunatumainia Hilo.”

³⁴ Ndipo jambo la kigeni likatukia. Nilizoea kuwa na maskini farasi, wa matandiko, nami ni—nilimwita Prince. Na jinsi nilivyompenda maskini farasi huyo mzee. Nilikuwa nikimpanda kila asubuhi, kabla ya kwenda shuleni, kutega mitego yangu. Ndipo nikamwona maskini farasi huyu mzee akinijia, akakiweka kichwa chake begani mwangu, na kulia. Basi nikampapasa. Nikasema, “Prince, nilijua ungekuwa hapa.” Kisha nikahisi kitu fulani kikiulamba mkono wangu. Ilikuwa ni maskini mbwa wangu wa kuuni. Aliniweka shuleni, akaninunulia nguo, kuwinda. Nikasema, “Prince, ama, Fritz, nilijua utakuwa hapa pia.”

Ndipo nikahisi kitu fulani kikitukia. Nilikuwa narudi.

³⁵ Hilo liliandikwa kwenye *Sauti* ya Wafanyabiashara. Ndipo mhudumu akaniandikia hivi majuzi. Akasema, “Nilifurahia ono hilo, Ndugu Branham. Lilisikika lote ni zuri sana mpaka ulipowataja farasi. Mbingu zimefanyiwa wanadamu. Hakuna kitu kama farasi Mbinguni.”

³⁶ Vema, nikasema, nikamjibu. Nikasema, “Ndugu, kamwe sikusema nilikuwa Mbinguni. Nilikuwa nikiuliza Yesu alikuwa wapi, na Yeye alikuwa angali juu zaidi.” Nikasema, “Lakini kama lingeweza kukusaidia kidogo, katika Kitabu cha Ufunuo, kinasema, ‘Wakati Yesu alipoondoka Mbingu za mbingu, Yeye alikuwa amepanda farasi mweupe.’ Nayo majeshi yote ya Mbinguni yalikuwa yakimfuata, wamepanda farasi weupe. Mnaona? Kwa hiyo hao walikuwa wakitoka Mbingu za mbingu.”

³⁷ Basi kile kilichonifanya kujisikia vizuri sana, hapo nilipoanza kurudi, Yeye alisema, “Wote uliowahi kuwapenda, na wote waliopata kukupenda, Mungu amekupa.”

³⁸ Siku moja angavu, upande ule mwingine, itakuwa ni tofauti. Siwezi tu. . . Kamwe hamwezi kuthubutu, enyi watu, kupakosa mahali hapo. Msifanye hivyo. Lolote ufanyalo, hakikisha. . . Usiogope. Hakuna haja ya kuogopa. Hakuna kitu cha kuogopa.

³⁹ Loo, nilipowazia kurudi, lilinihuzunisha. “Hivi itanibidi kurudi tena? Itanibidi kurudi, kwa yale niliyoogopa kuwa?” Mnaona? Ndipo tunapokuja kwenye mwili uliofufuliwa, basi tutakula na kunywa. Wao hawakula na kunywa. Hawakuwa na haja ya kula na kunywa. Hawakuwa wakienda popote, wala hawakuwa wamechoka. Ilikuwa ni ninii tu... Hakuna neno ningaliweza kutumia. Ilikuwa kamilifu; hilo halingelifanya. Limepita kile ninachoita kikamilifu. Wa—walikuwa tu wamewasili, jambo ndilo hilo, ma—mahali hapo, na ilikuwa ni ajabu sana.

⁴⁰ Kwa hiyo, loo, sikilizeni, marafiki. Na—nafikiri nina akili timamu, na mimi—mimi—mimi najua linasikika lisilo kawaida. Lakini kamwe sijaweza, wala kamwe sijajaribu, kuwaelezea watu mambo haya. Mambo mengi ambayo... Limepita kueleza. Nawe ungezivuruga tu nia za watu. Lakini kama ningeweza, na kujisikia nilieleze, lingekuwa ni la kushangaza sana.

⁴¹ Lakini angalieni hili. Ninasema hili. Msiogope. Kifo ni sanamu ya kutishia tu, ikijaribu kukuzuilia kitu fulani. Jamani, ni adhimu sana! Ni zaidi ya chochote ungaliweza kuwazia. Si ajabu Biblia ilisema, “Jicho halijaona, sikio halijasikia, wala hayajaingia katika mioyo ya wanadamu yale Mungu aliyowawekea wale wampendao.” Loo, kuangalia tu ng’ambo ya pazia la wakati! Halafu, nimejaribu kwa nguvu kuliko hapo awali maishani, kujaribu kuwaleta watu kwa Kristo, tangu wakati huo. Huwezi kuthubutu kulikosa. Usifanye hivyo. Hakikisha kwamba uko sawa na Mungu, ndipo mambo mengine yatakuwa sawa.

⁴² Sasa, ninayo muhtasari kidogo tu ulioandikwa hapa chini, niliofikiri ngingezungumzia kidogo usiku wa leo. Nami nafikiri kesho usiku tutakuwa huko juu kabisa, yapata maili ishirini kutoka hapa, ama zaidi. Mesa, ninaamini ndiko. Mesa. Huko ni Mesa? Mesa. Halafu kesho yake usiku huko Tempe, Tempe. Nami ninayo ratiba mfukoni mwangu hapa, kutoka kwa karatasi Ndugu Williams aliyonipa. Lakini, nimekuwa na shughuli nyingi sana, kamwe sijaiangalia bado. Billy huja tu na kunichukua, na kasema, “Tunaenda *fulani-fulani* na *fulani-fulani*,” nasi hapa tunaenda. Kisha naja huku, naye anajaribu kunikaba.

⁴³ Sasa, kila mtu anajisikia kubarikiwa sana? Semeni, “Amina,” kama mnajisikia. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vizuri sana. Hilo ni sawa. Sasa, hebu tuvinamishe tu vichwa vyetu sasa.

⁴⁴ Kama vile, ndio kwanza tuninii, maskini ucheshi wetu mdogo na matamshi. Sisi ni watoto, nasi tunakusanyika na kuzunguma kama watoto. Nasi... Hata Mungu anao ucheshi, mwajua.

⁴⁵ Kwa hiyo na tuinamishe vichwa vyetu sasa na kuzungumza na Yeye kabla hatujalisoma Neno Lake. Huku tumeinamisha

vichwa vyetu, kunao wale humu ndani walio na hitaji la maombi? Na ijulikane kwa mkono wako ulioinuliwa. Mungu akubariki. Na tuinamisha vichwa vyetu sasa.

⁴⁶ Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja katika Uwepo Wako sasa tunapoviinamisha vichwa vyetu na mioyo yetu katika unyenyekevu. Tunakaribia kwa imani, kupita mwezi na nyota, kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, kwa sababu tuna hakika kwamba kama tukija katika Jina Lake kwamba Wewe utatusikia. Tutakubalika Mbele Zako kwa Jina Lake. Ni majaliwa ya jinsi gani hayo, kujua ya kwamba tumekubalika Mbele za Mungu, kwa Jina la Yesu Kristo.

⁴⁷ Na Yeye alitwambia, Baba, ya kwamba lolote tuliloomba katika Jina Lake, kwamba Wewe, katika wingi wa rehema na neema Zako, ungetusamehe dhambi zetu na ungetujalia shauku zetu. Baba, tunashukuru sana kwa jambo hilo. Hakuna kitu kingine tungaliweza kuwazia, ambacho kingekuwa ni majaliwa ya juu zaidi, kuliko kuwa na majaliwa haya.

⁴⁸ Yangukuwa ni majaliwa kwetu sisi raia wa Marekani kumwendea rais wetu. Na yote yangalitulazimu kufanya, kupitia, tupate kumwendea rais kwa muda kidogo tu wa wakati, kuchukua muda kidogo wa ratiba yake yenye shughuli nyingi. Ingetulazimu kupitia ofisi nyingi, na—na kila njia, tupate kuja, na itatubidi kutoa sababu zetu, na—na ingebidi tuchunguzwe kabla hatujapata majaliwa hayo.

⁴⁹ Lakini, kuliwazia hilo: Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, anatungojea tumwendee. Sisi, wenye dhambi wasiostahili, Yeye anatungojea tumwendee katika Jina la Bwana Yesu, pamoja na hakikisho kwamba tutapewa tunayoomba, kama tunaweza tu kuamini kwamba tutapewa. Halafu, tungeyachunguza maombi yetu kwa makini sana na kujua kwamba tusingenena kijinga wala kuomba kijinga. Na kama tukifanya hivyo, tunaomba ya kwamba utusamehe, Bwana.

⁵⁰ Nasi tunaomba rehema usiku wa leo juu ya kila mmoja wa mikono hii iliyoinuliwa. Jalia wapewe haja zao, Bwana. Jalia wahisi hakikisho moyoni mwao sasa hivi, kwamba, wakati tukiwa katika Uwepo Wako, kwamba, tunapoyafungua macho yetu na kuviinua vichwa vyetu kutoka mavumbini, ambayo kutoka kwake Wewe ulitufinyanga, jalia tuhisi hakikisho hilo lililotiwa nanga kwamba tumepewa kile tulichoomba.

⁵¹ Tungeomba kwa ajili ya wale, Bwana, labda katika jengo hili usiku wa leo, ambao hawajawahi kuingia katika Uwepo Wako, kwa njia ya maombi, kuomba msamaha kwa ajili ya dhambi, jalia huu uwe ndio usiku ambapo jambo fulani litasemwa, ama jambo fulani kufanywa, ama matendo fulani ya Roho Mtakatifu ambayo yataifanya mioyo yao kutetemeka na kuomba neema hiyo inayosamahe.

⁵² Waponye walio wagonjwa. Bwana, tunaomba kwamba Wewe utawajalia, usiku wa leo, hakikisho ya kwamba maombi ya imani sasa yanaombwa. “Nayo yatamwoko mgonjwa.” Kwa kuwa tungeweza kusema, na kuongezea hili, kwamba hiyo ni BWANA ASEMA HIVI, kwa kuwa imeandikwa katika Neno la Bwana.

⁵³ Sasa, Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utabariki matamshi haya madogo yaliyotolewa hapa leo hii kwa ajili ya Neno Lako. Vuta kutoka somo hili muktadha kwa kila moyo. Na kama nikishindwa kwa njia yoyote, Bwana, na kuukosa upako wa Roho Mtakatifu, jalia Yeye katika neema ya Kiungu aende pamoja na Neno na kuliweka katika moyo ambamo lilipaswa kuwa. Basi tujalie usiku wa leo tuone mkono wa Mwenyezi ukinyoshwa kote kwenye jengo hili, na kufanya mambo ambayo yangekuwa ni mengi zaidi ya yale yote tungeweza kufanya ama kuwazia. Tutakapoondoka usiku wa leo na kwenda katika makazi yetu mbalimbali, jalia tuweze kusema kama wale waliotoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo aliposema nasi njiani?” Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

⁵⁴ Sasa, kidogo watu wengi huwa wanaandika, na fungu la maneno ambalo mhudumu anatumia. Na mimi, kama mkitaka sasa, ningetaka kusoma sehemu mbili katika Maandiko Matakatiifu. Hizo ni, katika Mwanzo mlango wa 22, tutaenda kwanza na kusoma. Na halafu katika Yohana Mtakatifu 12:32, tutasoma kwa ajili ya sehemu ya pili ya Maandiko. Sasa, katika Yohana... Katika Mwanzo 22, tunaanza na kifungu cha 7 cha mlango wa 22.

Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, Babangu! Naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?

Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka ya kuteketezwa, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja.

⁵⁵ Na sasa katika Yohana Mtakatifu 12:32, tunasoma Maneno haya kutoka kwenye midomo ya Bwana wetu.

Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote kwangu.

⁵⁶ Na sasa kwa ajili ya somo ambalo ningetaka kulizungumzia, juu ya hili, ni, “Kuikubali njia ya Mungu iliyowekwa kwa ajili ya wakati wa mwisho.” Hebu nilinukuu hilo tena, kwa sababu, kwenye kanda, ninaamini wanazinasia Jumbe hizi, na kwenye kanda tulizo nazo, mahubiri mia tano ambayo nadhani nimehubiri, yanacho kitu kinachofanana na hilo, bali silo hili hasa. *Kuikubali Njia Ya Mungu Iliyowekwa Katika Wakati wa Mwisho.*

⁵⁷ Mwajua, kunazo njia nyingi ambazo—ambazo watu hupitia, bali kweli kunazo njia mbili tu ambazo mwanadamu anaweza kupitia, hizo ni, njia sahihi na njia mbaya. Nasi sote hapa, usiku wa leo, tuko kwenye moja ya njia hizo, iliyo sahihi ama iliyo mbaya. Hakuna njia ya katikati. Yesu alisema, “Huwezi kumtumikia Mungu na *mamoni*,” ikimaanisha, “ulimwengu.” Ama tuko sahihi ama si sahihi.

⁵⁸ Na sasa kama tutaondoka tu kwenye njia yetu wenyewe, ndiyo njia pekee tunayoweza kuingia katika njia ya Mungu. Naye Mungu amefanya njia iliyowekwa kwa ajili ya kila kitu. Yeye ameiweka njia. Basi mahali tunapoingia katika matatizo, ni kwa kutoifuata njia hiyo, na—na kuingiza ndani Yake njia zetu wenyewe. Na hiyo inasababisha upotovu. Na kitu chochote kilichopotoshwa si—si cha kutegemewa. Kwa hiyo, Mungu anayo njia. Basi hebu tuangalie tu baadhi ya njia Zake.

⁵⁹ Hebu tuchukue kitu fulani katika maumbile. Kwa sababu, maumbile yalikuwa ndiyo Biblia yangu ya kwanza. Ninajua Mungu ni Muumba, na Yeye aliumba maumbile. Na Yeye huishi katika viumbe Vyake, katika maumbile.

⁶⁰ Hebu tuchukue, kwa mfano, mti. Ndio kwanza nisimame chini ya mmoja, muda mchache uliopita huko nje, ama Billy alisimama, nao una matawi juu yake. Nami niliona majani yakipukutika. Sasa, kamwe hatujaweza, wala kamwe hatutaweza, kupata njia bora kwa mti kuyaficha maisha yake kote katika majira ya baridi kali, kuliko njia aliyoiweka Mungu kwake kuuficha uhai wake.

⁶¹ Sasa, vipi kama tungalijaribu kutengeneza njia nyingine mbali na njia ya kawaida iliyowekewa huo mti? Vipi kama kila Agosti ama Septemba, hasa kwenye nchi ambamo mimi natoka, huko Kaskazini, kama ingetulazimu kwenda kwenye shamba la matofaa na kuchukua namna fulani ya cho—ya chombo na kukiweka kwenye huo mti, yapata Agosti baada ya matofaa kuiva, na kutoa uhai kutoka kwenye mti huo na kuupeleka katika mahali pazuri penye joto, na kuuweka kote katika majira ya baridi kali, huo uhai, utomvu ulioondolewa kutoka kwenye mti huo, na kuuweka katika chombo kizuri chenye joto na kuuhifadhi hata majira ya Kuchipua, kisha kuuchomeka tena kwenye ule mti? Mwajua, hilo halingefanya kazi. Kamwe haitakuwa hivyo. Na kujaribu kufanya hivyo kungeuua tu huo mti.

⁶² Lakini Mungu anayo njia ya kuutunza uhai huo kote katika majira ya baridi kali. Mungu aliweka njia. Akijua kwamba majira ya baridi kali yataujia huo mti, Yeye aliuwekea njia. Nilikuwa na majaliwa ya kumwongoza kafiri mwenye umri wa miaka sabini na mitano kwa Kristo, kwa jambo hilo, sio muda mrefu uliopita.

⁶³ Bw. Wood, jirani yangu, naye alikuwa ni wa imani ya Shahidi wa Yehova. Naye alikuwa na mvulana aliyekuwa kiwete, alikuwa na mguu uliokunjamana chini yake. Naye mke wake, ninaamini, alikuwa ni wa—wa kikundi cha Anderson cha Church of God. Nao wakaja Louisville, Kentucky, ambako waliishi katika mahali padogo panapoitwa Crestwood, yapata maili thelathini kutoka Louisville.

⁶⁴ Basi katika mkutano kule kwenye ukumbi, walimwona msichana aliyekuwa na ugonjwa huu hapa, kwamba, anageuka kuwa chokaa ama jiwe. Naye alikuwa, tayari umempooza, juu sana kwenye nyonga zake, hata hakuwa amesogea kwa, loo, miezi kadhaa. Nao ulitoka kwenye miguu yake. Aliombewa, usiku mmoja, na kesho yake alikuwa akikimbia juu-chini kwenye vipandio, upesi tu alivyoweza kwenda.

⁶⁵ Basi Bw. Wood akamleta mwanawe. Hakika, hakingia mkutanoni. Na mara baada ya hapo, nilipelekwa kwenye nchi za ng'ambo, nikaenda huko kwa ajili ya Bwana wetu. Basi niliporudi nilikuwa na mkutano huko kwenye... huko Ohio, naye akamleta huyo mvulana, jina lake David. Naye alikuwa ameketi nyuma kabisa, loo, karibu nusu jengo la mji.

⁶⁶ Naye Roho Mtakatifu akaingia na kusema, “Yupo mtu hapa usiku wa leo. Naye na mkewe wameketi huko nyuma kabisa.” Sijawahi kumwona maishani mwangu. Kisha kasema, “Huyo mtu, jina ni Wood. Yeye ni mkandarasi. Anaye mvulana kiwete aliyekuwa na polio, iliyokunja mguu mmoja chini yake. Bali, BWANA ASEMA HIVI, mvulana huyo ameponywa.”

⁶⁷ Yeye akiwa hajazoea kitu kama hicho, mvulana huyo aliketi pale kwa kitambo kidogo. Ndipo baada ya kitambo kidogo, mama yake akasema, “David, mbona usijaribu kusimama?” Basi aliposimama, huo mguu ulikuwa ni wa kawaida kama huo mwingine.

⁶⁸ Mtu huyo akauza biashara yake akaja huku, jirani yangu. Loo, yeye ni ndugu mpendwa sana! Hivi majuzi asubuhi wakati alipojua nilikuwa nikija huku kwa muda ulioongezewa, yeye ni... Kwenye mapambazuko, nilipotoka nyumbani, huyo hapo, amesimama barabarani, akilia namna *hiyo*; akiomba lifti, kana kwamba ataenda pamoja nami. Ndipo akanikumbatia kisha akatolemka uchochoroni. Ndugu mzuri sana! Amekuwa ni rafiki yangu kabisa.

⁶⁹ Tulikuwa huko chini katika jimbo la Kentucky, tukiwinda kuchakulo, yapata miaka mitatu iliyopita. Na kukawa kukavu kabisa. Na sasa, ikiwa yeyote wenu ninyi watu wa mashariki mnajua kuchakulo wa kijivu ni nini, yeye... Bingwa wa kutoroka Houdini si mweledi, kwake, wakati ametishwa. Kwa hiyo, ninapenda kuwawinda, kwa hiyo tunawawinda kwa bunduki ya .22. Nasi tulikuwa tumewinda. Nilikuwa kwenye likizo yangu yapata majuma mawili, nasi tulikuwa tukipiga

kambi huko nje. Nako kulikuwa kukavu sana. Nawe ungeweza tu kutembea kupitia mwituni na kuvunja ja—jani, naye jamaa huyo mdogo, loo, jamani, whiu, kamwe huwezi kumwona. Ameenda.

⁷⁰ Kwa hiyo Ndugu Wood akasema, “Ndugu Branham, ninajua ma—mahali hapa chini palipo na vibonde.”

⁷¹ Ni wangapi wanaojua kibonde ni kitu gani? Vema, mmetoka sehemu gani ya Kentucky? Na hivyo ndivyo wanavyokiita huko chini Kentucky. Hapa chini, ninaamini mnakiita genge ama kitu fulani, ambako maji hutiririkia tawi la mto. Nawe unaingia kwenye sehemu hizo zenye kilindi, na zingali na unyevu, nawe unaweza kutembea pasipo kusababisha kelele.

⁷² Akasema, “Ila mzee huyo ni kafiri, na, loo, yeye anawachukia wahubiri.” Nami nilikuwa kwenye nchi hiyo mara moja tu hapo awali, na hiyo ilikuwa ni kwenye mkutano.

Nami nikasema, “Vema. Wewe, wewe unamfahamu?”

Akasema, “Anamfahamu baba yangu vizuri sana.”

⁷³ Nikasema, “Twende tukamwulize, kwa sababu hatufanikiwi hata kidogo hapa.”

⁷⁴ Basi tukaenda kule katika maskini gari lake, na kupitia misituni, na kushuka chini kwenye vilima. Loo, jamani! Hatimaye tukafika mahali padogo. Basi kulikuwako na wazee wawili wameketi chini ya mtofaa. Ilikuwa karibu tarehe 20 Agosti.

⁷⁵ Basi akatoka kwenye gari, akaenda pale, na akasema, “Jina langu ni Wood.” Kasema, “Mimi ni Banks Wood.” Akasema, “Sijui kama ingekuwa ni sawa kama tukiwinda katika eneo lako.”

Akasema, “Wewe ni mvulana wa Jim Wood?”

⁷⁶ Sasa, baba yake ni mfasiri wa Mashahidi wa Yehova, ama alikuwa. Nayo familia nzima ilimjia Kristo, kila mmoja, kwa maono. Kila mmoja, nawaambia yale hasa yangetukia, nayo yakatukia vivyo hivyo. Loo, laiti ningesimama na kuwasimulia hadithi ya familia hiyo tu, jinsi walivyoingia. Kila mmoja wa hao watoto katika Ufalme wa Mungu sasa, amebatizwa kwa Roho Mtakatifu.

⁷⁷ Na kwa hiyo wakati Banks alipoukubali, nanii wake... jamaa zake wote walimfukuza. Hivyo tu. Alikuwa nje.

⁷⁸ Lakini, mmoja baada ya mwingine, kila mmoja wao akipitia kule, kumsalimia “aloo,” Roho Mtakatifu angewashika na kuwaambia mambo, ndipo wangeingia. Ndipo wangeenda na kumwambia mwingine. Ndipo angekuja, Yeye angemwambia jambo fulani, naye angekuja. Na hivyo ndivyo familia nzima ilivyomjia Kristo. Na kwa hiyo wakati tulipopata... kutoka kwa ninii...

⁷⁹ Alitoka kwenye gari, akamwambia huyo mtu. Akasema, “Wewe ni mwana wa Jim Wood?”

Akasema, “Naam.”

⁸⁰ Kasema, “Jim Wood ni mtu mwaminifu. Naam, bwana. Karibu. Winda utakako.”

⁸¹ Akasema, “Asante.” Kasema, “Nilikuja pamoja na mchungaji wangu.”

⁸² Akasema, “Wood, wataka kuniambia umekuwa duni sana hata inakulazimu kubebana na mhubiri popote uendapo?”

⁸³ Nikafikiri karibu wakati ulikuwa umewadia kwangu kutoka nje. Kwa hiyo nikatoka kwenye gari, nikatembeatembea. Loo, jamani! (Ninyi ndugu huwinda. Wawindaji wenzangu, ninajua mko humu ndani.) Na jinsi nilivyokuwa nimejawa na damu na mchafu, na masharubu marefu *hivi*, mwajua; sikuwa nimeoga kwa majuma mawili, na, loo! Kwa hiyo nikatoka kwenye gari na kuwajongea pole pole. Ndipo akaniangalia juu chini, mara mbili ama tatu. Nadhani aliwazia, “Ati mhubiri!”

Nikasema, “Mu hali gani?”

Naye akasema, “U hali gani?”

⁸⁴ Na kwa hiyo Bw. Wood akaanza kunitambulisha kwamba mimi ni nani, nanii wangu...mchungaji wake. Naye akasema...

⁸⁵ Kabla hajapata nafasi kufanya hivyo, yule mzee akasema, “Vema,” akasema, “Nitakwambia sasa hivi.” Akasema, “Mimi—mimi ninadhaniwa kuwa kafiri. Sina haja sana nanyi jamaa, mnaojiita wahubiri.”

Nikasema, “Naam, bwana. Vema.” Nikasema, “Hayo ni maoni yako.”

Naye akasema, “Vema, wajua, mimi ni kafiri.”

⁸⁶ Nikasema, “Siamini hilo lingekuwa linafaa kujivunia. Sivyo?”

Akasema, “Vema, nafikiria halifai.”

⁸⁷ Kwa hiyo nikasema, nikawazia moyoni mwangu, “Bwana, kama kamwe utanisaidia, nisaidie sasa.”

⁸⁸ Kwa hiyo mzee huyo mwingine aliyeketi pale, kamwe hakusema chochote. Maskini kofia za kale ukingo mpana, sijui nini... Mnajua ilivyo, imesokotwa kwa nyuzi za kitani, mwajua. Na kwa hiyo wakaketi pale kidogo.

⁸⁹ Na kwa hiyo akasema, “Unajua nilicho nacho dhidi yenu ninyi jamaa? Mnabwekea mti mwingine.”

⁹⁰ Ni wangapi wanajua maana ya hilo, “kubwekea mti mwingine”? Huyu ni mbwa mwongo, mwajua, anayebwekea mti mwingine. Mnyama amekwisha kuondoka pale. Hakuna kitu huko juu. Mnaona?

91 Kwa hiyo akasema, “Ninyi jamaa mnabwekea juu ya mti. Hakuna kitu huko,” kwa maneno mengine. “Mnazungumza juu ya Mungu, na hakuna kitu kama Mungu.”

“Vema,” nikasema, “hakika, tunaamini hilo.”

Akasema, “Vema, huenda mkaamini, lakini mimi siamini.”

Nikasema, “Vema, hilo ni sawa.”

92 Ndipo akasema, “Unaona lile dohani pale juu ya kilima?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

93 Kasema, “Nilizaliwa huko juu.” Kisha kasema, “Baba yangu alijenga mahali hapa hapa chini. Tuliamia hapa wakati nilipokuwa na umri wa kama miaka kumi na sita. Baada ya kifo cha baba yangu, nikapachukua mahali hapa. Nimeilea familia yangu. Nimekuwa hapa miaka sabini na sita ama sabini na minane, ama kitu kama hicho.” Akasema, “Daima nimetafuta, kila siku, kote angani. Nimetafuta kote mwituni. Nikatafuta kote shambani. Wala kamwe sijaona chochote kinachofanana na Mungu.”

Nikasema, “Vema, hiyo ni mbaya sana.”

94 Naye akasema, “Hiyo ndiyo sababu nafikiri kwamba ninyi jamaa mnabwekea juu ya mti mwingine.”

95 Nikasema, “Naam, bwana.” Ndipo basi jambo fulani likatukia. Nikaangalia juu ya mti. Nikaangalia chini, na pale yalikuwapo matofaa juu ya mti. Nikasema, “Ni sawa kama nikichukua moja ya hayo matofaa?”

96 Akasema, “Karibu. Manyigu wanayala.” Mnajua manyigu ni nini, nina hakika.

97 Kwa hiyo ni—nikainama, nikaokota moja ya hayo matofaa, nikalisugulia kwenye mguu wangu wa suruali, mwajua. Ndipo nikaliuama. Nikasema, “Hilo ni tofaa tamu sana.”

Akasema, “Naam, hilo ni tamu.”

Nikasema, “Mti huo una umri gani?”

98 Akasema, “Niliupanda pale. Hebu tuone, una miaka arobaini na saba, arobaini na minane, kitu kama hicho.” Kasema, “Nilipanda kichipukizi kidogo.” Kasema, “Nilikitoa mahali fulani, mahali pengine mbali, ndipo nikakileta hapa.”

Nikasema, “Naam, bwana.” Kisha nikasema, “Unazaa kila mwaka?”

99 “Kila mwaka unazaa matofaa mazuri.” Kasema, “Tunaweka koponi matofaa mengi kutoka pale.”

100 Ndipo nikasema, “Vema, hilo ni zuri sana. Nina furaha kusikia hilo.” Ndipo nikasema, “Unajua, hapa ni tarehe kumi na tano tu ya Agosti.” Nikasema, “Ni karibu tisini kwenye kivuli wakati wote.” Nikasema, “Ni ajabu kwamba majani hayo yote

yanapukutika kutoka kwenye mti huo, huku hatujawa na jalidi yoyote.”

¹⁰¹ Naye akasema, “Loo, hiyo ni—hiyo ni, utomvu umerudi kwenye mzizi.”

“Loo,” nikasema, “ndivyo ilivyo?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Kisha unarudi kwenye mzizi, kwa sababu gani?”

¹⁰² Akasema, “Vema, kama ungekaa kule juu, baridi kali ingeuua.”

Nikasema, “Kuuu nini?”

¹⁰³ Akasema, “Huo mti. Chembe ya uhai imo katika utomvu huo, unashuka chini na kujificha mizizini.”

Nikasema, “Loo.” Nikasema, “Sasa, hiyo... Vipi kuhusu...”

Akasema, “Vema,” akasema, “hilo si jambo lisilo la kawaida.”

Nami nikasema, “La, la. Hilo ni tendo tu la maumbile.”

¹⁰⁴ Akasema, “Wajua, nataka kukuambia jambo fulani.” Akasema, “Kabla hujaendelea mbele zaidi, ninataka kusema jambo hili. Kwamba nilisikia kumhusu mhubiri mmoja wakati mmoja, ambaye ningetaka kumsikia mara moja, kama akipata kuja kwenye nchi hii tena, ninataka kumsikia.”

Nikasema, “Loo? Hilo ni zuri,” nikasema.

¹⁰⁵ Akasema, “Yeye alikuwa huku Acton yapata miaka miwili iliyopita kwenye uamsho huko kwenye—kwenye uwanja wa maonyesho wa Methodist huko nje, ule uwanja wa kambi wa Methodist.”

¹⁰⁶ Ndipo Banks akaangalia. Nikamgeukia Banks, mimi... Huyo ni, Ndugu Wood. Nikasema...

¹⁰⁷ Naye akasema, “Nasahau jina la mtu huyo lilikuwa lipi sasa.” Kasema, “Unajua, hakuwa amekuja katika nchi hii hapo kabla.” Tena kasema, “Bikizee,” mtu fulani, “anaishi hapa juu yapata maili moja, juu ya kilima.” Akasema, “Alikuwa yuafa kwa kansa. Nao walimpeleka Louisville, maili mia moja na ishirini, nao madaktari wakampasua. Nalo tumbo lake lote lilikuwa limefunikwa, matumbo na kadhalika, na kansa. Nao wasingeweza kumfanyia lolote.” Naye akasema, “Basi wakaleta... wakamshona na kumrudisha. Basi mimi na mke wangu tulikuwa tukipanda kule kila siku. Wala wasingeweza kumwinua tena; ilitubidi tu kuvuta shuka la kulalia ili kumbadilishia malazi.” Ndipo kasema, “Tumekuwa tukienda kule kwa majuma kadhaa.” Alikuwa akitarajia yeye kufa usiku wowote, au wakati wowote. Kisha kasema, “Dada yake anaishi

huko nyuma kwenye kijito kingine.” Mwajua, hivyo ndivyo unavyoyatambulisha, kule chini. Si barabara; ni kijito. “Huko kwenye kijito kingine.”

¹⁰⁸ Nimemsikia mtu fulani akicheka. Kumejaa Wakentaki watupu hapa ndani. Huko...Vema, nilizaliwa kwenye kile wanachokiita Little Renox huko chini. Babu yangu aliishi kwenye Big Renox, unaomwaga maji yake katika Bombshell. Kijito cha Bombshell huja moja kwa moja kwenye Little Renox, na kutiririkia kwenye Kivuko cha Casey, na unabubujikia kwenye Mto Cumberland. Sasa, hiyo ni ng'ambo tu ya Kigongo cha Greenbrier. Hapo ndipo mama yangu alipozaliwa, juu ya Kigongo cha Greenbrier.

¹⁰⁹ Basi akasema, “Mwanamke huyu aliishi kule ng'ambo mahali pengine.” Kisha kasema, “Hiyo ni kama maili ishirini kutoka hapa. Naye alikuja usiku huo, na alikuwa ameketi huko nyuma kabisa ya huo uwanja wa kambi.” Ndipo kasema, “Mhubiri huyu, wakati alipokuwa pale, yeye huwaombea wagonjwa.” Kisha kasema, “Yeye alikuwa akiwaambia watu kwamba wao ni nani, na yote kuwahusu.”

¹¹⁰ Kasema, “Mwanamke huyu alifika amechelewa, naye hakupata moja ya hizo kadi walizokuwa wanasambaza.”

¹¹¹ Kisha kasema, “Mhubiri huyu alimgeukia, akamwambia, kasema, ‘Unajua, wewe, mama unayeketi huko nyuma, wewe ni *Fulani-wa-fulani*. Na usiku wa leo ulipotoka nyumbani, uliweka lesu ndogo kwenye kitabu chako cha mfukoni, chenye mchoro wa samawati pembeni mwake.’ Kasema, ‘Nawe unaye dada jina lake *Fulani-wa-fulani*.’ Kisha kasema, ‘Yuafa kwa kansa ya tumbo. Ndio kwanza nilione katika ono. Sasa, ichukue lesu hiyo, uende ukaiweke juu yake. Na, BWANA ASEMA HIVI, atapata afya.’”

¹¹² Akasema, “Naye mama huyo... Usiku huo, tulisikia kelele iliyo mbaya sana, huku juu ya kilima. Nilidhani walikuwa na Jeshi la Wokovu huko juu,” akasema, “yapata usiku wa manane. Nasi tukafikiri maskini bikizee huyo amekufa.”

¹¹³ Kisha akasema, “Unajua nini? Mimi na mke wangu tulipanda tukaenda kesho yake, tuone kama tungeweza kuwafariji, mapema asubuhi. Naye huyo ameketi mezani, akiwa na birika la kahawa, akimimina tu kahawa, naye pamoja na mumewe walikuwa wakila sambusa za tofaa nusu-mwezi zilizokaangwa kwa ajili ya kiamshakinywa.” Nikasema...

¹¹⁴ Ni wangapi wanaojua sambusa za tofaa nusu-mwezi ni nini? Mwajua, niko nyumbani sasa. Hizo zilikuwa tu... Ninazipenda, nami napenda zilizopakwa sukari ya rojorojo ya mtama. Nami nimetafuta kote mahali hapa nipate sukari ya rojorojo ya mtama. Na kama nikirudi hapa tena, nitakuja na ndoo nzima, maana ni vigumu kwangu kuendelea bila hiyo. Nanyi mwajua, ni—ninatumia nyingi, maana mimi kwa namna fulani ni Mbaptisti, mwajua. Si—si—siamini katika kuzinyunyizia hizo

keki. Ninazibatiza tu zote tena, vizuri sana. Na mimi...Kwa hiyo ninazimwagilia sukari ya rojorojo, nzito.

Kwa hiyo basi akasema, "Alikuwa akila hizo." Nikasema...

Nikawaza, "Huu ndio."

Nikasema, "Sasa, humaanishi hilo."

¹¹⁵ "Vema," akasema, "panda juu kule ukajionee mwenyewe." Kasema, "Hiyo imekuwa ni miaka miwili iliyopita." Kisha kasema, "Si kwamba tu anajifanyia kazi yake mwenyewe; yeye hufanya kazi za jirani yake." Sasa, mnaona, yeye alikuwa akinihubiria wakati huo.

¹¹⁶ Mwajua, mama yangu alikuwa akisema, "Mpe ng'ombe kamba ya kutosha, atajinyonga mwenyewe." Kwa hiyo hiyo ni karibu kweli. Alijinasa kwa maneno yake mwenyewe, wakati huo, aliposema—akasema, "Panda huko juu ukajionee."

¹¹⁷ Nikasema, "Sasa, angalia, bwana. Unamaamisha madaktari walimpasua mwanamke huyo wakampata na kansa?"

"Hiyo ni kweli."

¹¹⁸ Nami nikasema, "Kisha wakamshona? Halafu wataka kuniambia ya kwamba mtu huyo kule, maili kumi na tano kutoka hapa, alimwona mwanamke huyo na kusema yale hasa yangetukia watakapoweka hiyo lesa juu yake? Naye mwanamke huyo akapona hiyo kansa?"

Kasema, "Panda moja kwa moja kule juu. Nitakwambia jinsi ya kufika kule."

¹¹⁹ Nikasema, "La, la. Ninachukua neno lako." Nikasema, "Ninachukua neno lako." Nikasema, "Naam, bwana. Naam."

¹²⁰ Nilikuwa nikila tofaa hili, mwajua, wakati wote, nikilitafuna. Nikasema, "Hilo ni tofaa tamu." Nikasema, "Ninataka kukuuliza swali. Ni kitu gani kilichoufanya utomvu huo kuondoka mtini na kushuka mizizini?"

¹²¹ "Mbona," akasema, "ilibidi ushuke, upate kuuhifadhi uhai wake kwa ajili ya majira ya baridi kali."

¹²² Nikasema, "Ndipo msimu ujao wa kuchipusha unarudi, ukikuletea vichane vingine vya matofaa?"

"Kweli."

¹²³ Nami nikasema, "Sasa nataka kukuuliza jambo fulani. Ni akili gani inayouongoza utomvu huo, inayosema, 'Aisee, ni msimu wa majani kupukutika. Shuka chini mizizini ukajifiche. Usipojificha, majira ya baridi kali yatakuua. Rudi chini mizizini ukae huko mpaka majira ya kuchipusha. Halafu basi joto likiingia na inakuwa ni sawa tu, sasa panda juu ukazae matofaa mengine kwa ajili ya jamaa huyu?' Sasa, unajua huo ni uhai wa mimea. Hauna akili yake wenyewe. Basi, niambie ni akili gani

inayoutuma uhai huo chini kwenye mzizi wa mti huo. Hauna akili yake wenyewe.”

Yeye akasema, “Hayo ni maumbile tu.”

¹²⁴ Nikasema, “Basi chukua ndoo ya maji, ukaiweke kwenye ile nguzo pale nje, uone kama maumbile yatayatelemsha katika msimu wa majani kupukutika, kisha yayalet katika msimu wa kuchipusha. Unaona? La, bwana. Ni kitu gani?”

¹²⁵ Sasa, kando kwa dakika moja. Ni njia ya Mungu iliyowekwa. Inatenda kazi tu njia ile Mungu anayoweka kwa ajili yake. Sauti ndogo inasema, “Shuka kwenye mizizi,” nao unashuka. Sasa, hufanya hivyo pasipo na akili yoyote. Inatupasa kufanya nini, wakati Mungu yuyo huyo anapozungumza nasi? Sisi, ila tunayo haki ya kukataa ama kukubali, na, zaidi sana, sisi hukataa. Mti hauwezi kukataa. Unajua zoezi moja tu, hilo ni, kumtii Bwana wake.

“Vema,” akasema, “Kamwe sikuwa nimewazia hilo hapo kabla.”

¹²⁶ Nikasema, “Hebu nikwambie. Wewe wazia hilo, muda mrefu, tunapoenda kuwinda. Ndipo nitakaporudi, wewe niambie ni kitu gani . . . ni kitu gani kinachouambia utomvu huo wa mti ushuke chini mizizini, na kukaa huko majira ya baridi kali, kisha urudi tena msimu ujao wa kuchipusha. Utakapojua ni akili gani inayoongoza uhai huo—huo wa mti, na kusema, ‘Shuka mizizini, kisha urudi,’ nitakwambia ni Akili ile ile iliyoniambia, ‘nenda kaiweke hiyo lesa juu ya yule mwanamke, naye atapata afya.’”

Akasema, “Kukwambia wewe?”

¹²⁷ Nikasema, “Naam, bwana.” Nikasema, “Jina la mtu huyo lilikuwa nani? Unakumbuka?”

Akasema, “Siwezi kulikumbuka.”

Nikasema, “Kwani halikuwa Branham?”

Akasema, “Ndilo hilo.”

Nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

¹²⁸ Hapo kwenye mahali hapo akasimama, akanishika mikono. Akasema, “Kwa mara ya kwanza maishani mwangu, ninaona unalomaanisha.” Nikamwongoza kwa Kristo.

¹²⁹ Mwaka jana nilikuwa huko chini. Ameshaondoka, akaaga dunia. Rehema za Mungu! Huyo hapo mke wake ameketi, chini ya mti, anamenya matofaa, kutoka kwenye mti ule ule. Nilijongea pale na kusema, “Naweza kwenda kuwinda?”

Akasema, “Haturuhusu uwindaji wowote.”

¹³⁰ Nikasema, “Samahani.” Ni—ni—nikasema, “Nilidhani nilikuwa na ruhusa.”

Akasema, “Kwani ulipata ruhusa kutoka kwa nani?”

Nikasema, “Mume wako.”

Naye akasema, “Mume wangu ameaga dunia.”

Nikasema, “Ameaga dunia hivi karibuni tu, sivyo?”

Kasema, “Naam. Kamwe hawapi watu ruhusa.”

¹³¹ Nikasema, “Nje chini ya mtofaa huu... Mwaka jana, nilikuwa huku chini, na tulikuwa tukizungumza juu ya mti huu.”

Akasema, “Wewe ni Ndugu Branham?”

Nikasema, “Naam.”

¹³² Akaiangusha ile sufuria ya tofaa. Akasema, “Ndugu Branham, yeye alikufa katika ushindi wa Yesu Kristo, ushuhuda wake wa mwisho.”

¹³³ Ni kitu gani? Kuona tu, sio kujaribu kupitia kwenye hisabati zote za jinsi linavyotukia, bali kitu kidogo rahisi tu, kumwangukia Mungu akiweka njia, na kitu fulani kikitumisha njia. Mnaona, Akili ile ile ambayo ingeuambia mti bubu, “Shuka ukajifiche uyaokoe maisha yako,” akili iyo hiyo Ndiyo iliyonionyesha ono la huyo mwanamke. Ndipo akalishika. Wala asingeweza kulikana, yeyote wao. Huo hapo ule mti umesimama, na huyo hapo yule mwanamke. Amina. Mnaona? Njia ya Mungu iliyowekwa!

¹³⁴ Wala hawajapata njia bora zaidi ya kifaranga kutoka kwenye ganda la yai, kuliko kulidonoa akatoka. Hawana njia yoyote bora. Sayansi kamwe haijaweza kutengeneza kitu kingine chochote. Kama ukilipasua hilo ganda, kumtoa, ingemwua. Atakufa. Hana budi kuifuata njia ya Mungu iliyowekwa, apate kuishi. Amina. Hilo linafanya kazi juu ya wanadamu, pia.

¹³⁵ Amapewa nyenzo. Hivi uliwahi kuona maskini kifaranga anapotoka kwenye ganda? Anacho cha ziada, maskini kidomo kwenye ganda lake, kikwaruzio kidogo cheupe. Naye jamaa huyo mdogo humo ndani, mara uhai unapoanza kuja, anaanza kukitikisa maskini kichwa chake. Huko kunafanya nini? Kikwaruzio hicho kidogo hulikwaruza hilo ganda, na kulifanya jembamba. Anapopata uhai mwingi zaidi kidogo, anaanza kugonga kwa kitu hicho kidogo. Basi akiisha kutoka kwenye ganda, hakihitaji tena, kwa hiyo kinaanguka tu chini.

¹³⁶ Nacho kitu kinachosababisha hilo, ni kinga ya ncha ya kidomo chake. Isingalikuwa hivyo, angekuwa na kidomo kilichoumbuka, wala asingeweza kuidonoa nafaka yake. Loo, jamani! Njia ya Mungu iliyowekwa ya kuishi! Mungu humwandaa, njia tu ya kutoka humo. Hakuna njia iliyo bora zaidi. Kitu kingine chochote kingemwua. Hana budi kupitia kwenye njia ya Mungu iliyowekwa. Sasa, kama ukijaribu kutengeneza njia nyingine ama kuwazia njia nyingine, utamwua.

¹³⁷ Hiyo ndiyo shida ya kanisa la Kikristo siku hizi. Limejaribu kukubali njia fulani iliyotengenezwa, badala ya kupiga na kutoboa njia yake, kuingia kwenye Ufalme wa Mungu. Limejaribu njia nyingine, nayo haitafanya kazi. Unamwua mgonjwa wako. Unamwua m—m—mtoto wako mchanga, mtoto mchanga wa Mungu, kwa kujaribu kujitengenezea njia fulani. “Loo, hakuna haja ya hii hapa boo-hoo na kulialia. Hakuna haja ya *haya* yote, *haya* yote.” Loo, naam, ipo. “Hakuna haja ya kufa huku.”

¹³⁸ Pasipokuwapo na kifo, hapawezi kuwa na uzazi. Kuzaliwa hutokana tu na kuwepo kwa mauti. “Punje ya ngano isipoanguka ardhini na kufa, hudumu peke yake.” Haina budi kuoza, na kuingia katika uharibifu, na halafu kutokana na uharibifu huo kunainuka uhai. Hakuna njia nyingine itakayofanikiwa. Haina budi kuoza kwanza, na kuharibika. Na hivyo ndivyo hatuna budi kuwa; kufa kwa nafsi zetu na kuzaliwa upya na Roho Mtakatifu.

¹³⁹ La, hawajapata njia yoyote bora kwa kifaranga kutoka kwenye ganda, kuliko kudonoa kikatoka. Hiyo ndiyo njia ya Mungu iliyowekwa kwa ajili yake, naye amepewa nyenzo kulifanya. Mungu asingeweza kuiweka njia pasipo kutoa kifaa kwa ajili yake. Kwa hiyo Yeye aliweka njia, kisha akatoa kifaa kwa ajili ya kifaranga kujiweka huru. Amina.

¹⁴⁰ Sasa, wala kamwe hawajapata njia bora zaidi kwa mabata na mabata bukini kuja kusini, kutoka kaskazini, kuliko kukusanyika kisha kuruka kwenda zao chini. Hakuna njia nyingine. Mnaona, kabla hawajaruka chini kusini, ama kuruka kutoka kusini kurudi kaskazini, wanakusanyika, kwanza. Kabla hawajaondoka kwenye maeneo yao ama nyumbani, kuhamia makao mapya, wanakusanyika. Nyuki hufanya jambo lile lile. Wanakusanyika. Hayo ni maumbile. Ni kitu gani? Wana uamsho. Wote wanakusanyika na kuja pamoja. Kamwe hujawahi kusikia kelele kama hizo maishani mwako.

¹⁴¹ Na kabla hatujaweza kuondoka kwenye makao haya, kuhamia mapya, hatuna budi kukusanyika katika uamsho.

¹⁴² Loo, hebu likaribie kundi la mabata na mabata bukini, kamwe hujawahi kusikia mapayo mengi hivi maishani mwako mwote. Wana nini? Uamsho. Wanajiandaa kuruka hewani. Amina.

¹⁴³ Hilo ndilo tunalohitaji leo hii, ni uamsho wa kukusanyika. Hakuna njia nyingine; sio uanachama. Mungu hahesabu wingi wa watu. Yeye huhesabu uaminifu katika njia Yake aliyoiweka.

¹⁴⁴ Sasa, kamwe hawajapata chochote cha kupachukua mahali pake. Kusingeweza kuwa na njia bora zaidi. Sasa, kwa mfano vipi kama sayansi ingesema, “Maskini vijibata. Hatutaki wakusanyike tena. Nasi tutawarushia wavu, kabla hawajakuwa tayari kukusanyika. Nasi tutawakusanya moja kwa moja

tuwaingize kwenye kizimba, nasi tutawabeba tuwapeleke kusini.”

¹⁴⁵ Hiyo ni kama vile, kuwaingiza kwenye dhehebu fulani ama kitu fulani, mwajua, kumweka kizimbani mahali fulani. Hiyo ni akiwa njiani kuelekea machinjioni. Yeye anajua anaenda machinjioni wakati anapoingia kizimbani. Lakini anapoiendea njia ya Mungu aliyoiweka, yuko mbali sana na hayo. Kwa hiyo, labda sikupaswa kusema hivyo. Sikulikusudia katika—katika njia ya kuwa kashfa dhidi ya dhehebu fulani. Lakini mnajua ninalomaanisha. Labda hayo ndiyo yote. . .

¹⁴⁶ Hiyo siyo njia ya kulitekeleza. Huwezi kujiingiza katika dhehebu, na kujiweka katika kizimba na kusema, “Mimi ni Mmethodisti, ama Mbaptisti,” ama mengine zaidi. Hilo silo. La, la.

¹⁴⁷ Huna budi kukusanyika. Hiyo ni kweli. Huna budi kufikia mahali unapoweza kujidonolea ukatoka.

¹⁴⁸ Hawa, wanakusanyika, nao wanaingia kwenye kizimba hiki. Na—na wakati wao. . . Wakifanya hivyo, wanajua wanaelekea machinjioni.

¹⁴⁹ Lakini, sasa, vipi kama ungaliwaweka wote, uwakusanye na kuwaweka kwenye kizimba, na kuwatelemsha kusini, uwafungulie. Halafu, kabla hawajakuwa tayari kukusanyika, uwarushie wavu juu yao. “Hatuamini katika siku za miujiza.” Mnaona? “Ninyi maskini mabata, hamwezi kuruka tena. Huko kulikuwa ni kwa ajili ya mabata wa wakati mwingine.” Mradi tu Mungu anamfanya bata, Yeye huwafanya wote namna ile ile. Na kama Mungu akiweka njia kwa ajili ya bata kupitia, hiyo ndiyo njia mabata wote watakapitia.

¹⁵⁰ Nanyi mnajua vile ingefanya? Hatimaye ingemuua huyo bata. Angekuwa mnyonge sana, mabawa yake hayangekua sawasawa. Asingeweza kuruka tena. Kama tu binamu yake wa ugani, tumbo tupu pasipo bata. Mnaona? Hana mabawa yoyote ya kujinyanyulia juu. Hiyo ni kweli. Mnaona? Angekuwa dhaifu kama binamu yake wa ugani, ndugu zake wa kimadhehebu wasioenda popote. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona? Hiyo ni kweli. Hivyo tu ndivyo angalikuwa, maskini mnyonge. Asingejua lolote kuhusu kuruka awe huru. Amina.

¹⁵¹ Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Tunajaribu kuwaingiza katika kizimba, na kuwaambia, “Siku za miujiza zimepita. Wala asingeweza kujiamini, miguu yake ikitoka ardhini. Ingemwua. Asingeweza kuishi muda mrefu sana.”

¹⁵² Lakini, mwajua, maskini bata huyo angesema, kama angaliweza kujibu, “La, asante.”

¹⁵³ “Loo, ni rahisi. Huna jambo la kufanya. Unaweza tu kufanya upendavyo.”

154 Angesema, “Asante. Mimi hufanya nipendavyo, kwa sababu kuna kitu fulani ndani yangu, kinachotenda kazi. Amina. Nami sina budi kufanya nipendavyo.” Na kila mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, kuna kitu fulani kinachotenda kazi ndani yake. Hana budi kuruka aingie mbinguni, mhemuko fulani, kitu fulani kinacholifanya halisi.

155 Maskini jamaa huyo hatimaye atakuwa kama kuku, ndege wa kufugwa. Kamwe asingeweza kuinyanyua miguu yake kutoka ardhini tena. Kwa hiyo kama kuku sikuzote angeendelea kuruka hewani, mbona, angeweza kwenda sawasawa. Angeweza kwenda mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini, na kuona mambo.

156 Na jambo lingine, mnaona, asingeweza kufanikiwa. Kwa sababu, akienda zake kutoka Canada, yeye huokota vitu vya aina mbalimbali, chakula ambacho asingeweza kupata kama ulikuwa umemweka kizimbani, ukimlisha tu mahindi wakati wote. Mnaweza kusoma katikati ya mistari? Ukimweka mle, kwa hiyo anajua tu Kanuni ya imani ya Mitume, inavyoitwa, na jinsi ya kwenda kwenye shule ya Jumapili, na hiyo ni karibu yote yaliyopo; kumlipa mhubiri, na kuishi jinsi atakavyo.

157 Lakini, loo, unapokuwa katika safari ya hewani, amina, unapokuwa katika safari ya hewani, unaokota mengi kuliko kanuni yako ya imani ya kimadhehebu. Unaokota vitamini, vitamini za kiroho zinazoujenga mwili ulio imara, uliojaa misuli, pamoja na manyoya ya mabawa yanayoweza kukunyanyua kutoka miguuni mwako na kukuonyesha mambo yajayo. Roho Mtakatifu, “Wakati Yeye, Roho Mtakatifu ajapo, Yeye atawaonyesha mambo haya, atawafunulia mambo haya ambayo nimewaambia; na mambo yajayo atawapasha habari zake.” Naam. La, usingeweza kumweka kizimbani na kumchukua. Isingefanya kazi. La. Kama ukimweka kizimbani, anaelekea machinjioni.

158 Wala mtu kamwe asingeweza kuchagua njia bora kuliko ile anayoweza. Huenda ukaenda na kusema, “Sasa, Bw. Bata, nitakwambia jambo fulani. Unapitia njia mbaya. Huna budi kupitia *hapa*, badilisha njia. Shuka uambae pwani *huku*, inakoelekea. Ni bora kuliko njia unayopitia.” Kamwe haitafanya kazi. La. La. Wanadhani wanajua njia bora kuliko njia ya Mungu waliyowekewa. Lakini, wanajua.

159 Ama, ungeweza kuwachagulia kiongozi bora kuliko kiongozi aliyetolewa na Mungu ambaye Mungu amewapa? Wala mwanadamu kamwe hataweza kuchagua askofu, wala dhehebu, wala kingine chochote kitakachopachukua mahali pa uongozi wa Roho Mtakatifu kwa Kanisa. Hakuna kitu kingine kingaliweza kulifanya. Njia ya Mungu iliyowekwa! Mungu aliwawekea njia, Kiongozi, Kiongozi aliyevuviwa.

¹⁶⁰ Naye kiongozi huyo amevuviwa. Mbona, nimewaangalia mara nyingi, ninapochukua safari ya mawindoni mapema, nikiwafuatilia kondoo ama kitu fulani ambapo inakubidi kwenda mapema, huko juu milimani. Hakujakuwa hata na jalidi. Labda, huko juu, theluji kidogo itaufunika mlima. Huo upepo baridi utapitia kote mlimani. Kunaye kiongozi asilia aliyezaliwa miongoni mwao. Atakimbia moja kwa moja penye lile ziwa namna hiyo, na kutoa mlio mara nne ama tano, na hapo hayo makundi yanakuja. Naam, bwana. Wote wanamtambua. Wanamtambua kwa mlio wake. Loo, jamani!

¹⁶¹ Mnajua yale niliyokuwa nikizungumzia jana usiku, baragumu ya Injili, kama ikitoa sauti isiyojulikana. Sauti yake haitoi isi-. . . Yeye hatoi sauti isiyojulikana. Hao ni mabata halisi. Wanajua sauti ya bata. Vipi kama ukimweka kanga mzee huko nje, ama bata mzinga? Mlio wake haungesikika sawa. Wao wanajua sauti ya kiongozi.

¹⁶² Nalo kanisa linapaswa kuijua. “Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake,” hao nao, msiwaruhusu kuongoza. “Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizua,” na wasiowapenda mabata hao wanaoruka juu. Mnaona? Mnaona ninalomaanisha?

¹⁶³ Wao—wao wanajua sauti ya Injili yao. “Kondoo Wangu wanajua Sauti Yangu.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “Mgeni hawatamfuata.” Mungu daima hulithibitisha kuwa ni kweli.

¹⁶⁴ Angalieni, sasa. Nao hawawezi kupata ninii. . . Usingeweza kuwachagulia. Vipi kama ulienda kule nje, nawe ukasema, “Loo, ngojeni kidogo, mabata wadogo. Hakika mmekosea. Huyu hapa bata dume mzuri mkubwa. Jamani, anaonekana wa kifalme miongoni mwenu. Basi sasa mnajua kile nitakachofanya? Nitamnyunyizia maji kidogo juu ya kichwa chake, nami nitamtawaza. Nitamfanya Bata Mfalme. Nami nitaweka taji juu yake, na kumvalisha tofauti kidogo, kusudi nyote mpatе kumtambua. Sikuzote mfuateni jamaa huyu hapa, kwa kuwa yeye ni mstaarabu.” Mwachilieni kwenye kidimbwi. Angeweza kutoa mlio kadiri atakavyo. Kila bata angempa kisogo, maana anatoa sauti isiyojulikana. Naam.

¹⁶⁵ Bali hebu maskini bata huyo aliyechaguliwa na Mungu kuwa kiongozi, hebu atoe mlio, ndipo mwone wote wakikusanyika kwa ajili ya uamsho. “Palipo na mzoga, ndipo watakapokusanyika tai.” Yeye anajua yote kuhusu jambo hilo. Mnaona? Kwa hiyo Yeye—Yeye anayo njia iliyowekwa. Nao mabata wanajua njia iliyowekwa. Ni vibaya sana kwamba mwanadamu haijui. Vema. Lakini hivyo ndivyo linavyotukia, sasa. Vema.

¹⁶⁶ Kama yeye ndiye kiongozi-bata aliyevuviwa, yeye atawaleta mahali pa Mungu palipowekwa kwa ajili yao. Na kama

tungesikiliza tu yale huyo Kiongozi asemayo, Roho Mtakatifu, Yeye ataturejesha moja kwa moja kwenye Neno tena. Hiyo ndiyo njia ya Mungu iliyowekwa. Tukiwa safarini hatuhitaji kanuni za imani na dhehebu, na magugu mwitu. Kuna nyasi fulani za bata na kadhalika ambazo tunapaswa kula, mabata wanapaswa, wakiwa safarini. Na kunacho chackula ambacho ninii... Kweli, ma—maua ya Mungu, viumbe wanaoelekea mbinguni wanachokula njiani, na hicho ni, “Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Mnaona?

¹⁶⁷ Bata huyo, kiongozi bata, atawaongoza kwenye mahali pa Mungu palipowekwa, moja kwa moja kabisa hadi Louisiana. Ambako, mmoja wa hawa wengine asingejua mahali alipokuwa akienda, ataruka huko juu na kuzunguka-zunguka.

¹⁶⁸ Nilikuwa nikisoma kwenye gazeti la *Life*, yapata miaka mitatu ama minne iliyopita, ambapo kulikuwako na bata dume la bukini aliyejitokeza pamoja na kundi moja huko juu. Naye alidai alikuwa ni kiongozi. Basi muda si muda mwajua, waliishia huko Uingereza, hawajawahi kurudi bado. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo inawabidi kuangalia ni aina gani ya bata ama dume wanayemfuata. Kwa hiyo wanasema, huko Uingereza... Hao watoa mlio wa Canada, pia. Nao wanafika huko Uingereza, na kote kote, wanakusanyika, bali hawajui njia ya kurudi. Loo, jamani!

¹⁶⁹ Ni vibaya sana kanisa lilicheza mchezo mwingi wa aina hiyo, pia, wakafuata wakaingia mahali fulani, hawajui jinsi ya kurudi. Kasema, “Vema, sisi... Nasikia kwamba nyanya alisema, mlolongo wa akina nyanya ulisema kwamba nyanya yake alisema, ya kwamba walikuwa wakifanya ibada za uponyaji kanisani. Siku hizo za miujiza zimepita,” unamwacha mtu akuongoze uingie kwenye njia mbaya. Afadhali uifuata njia ya Mungu iliyovuviwa, njia ya pekee.

¹⁷⁰ Tazameni, maskini bata huyu, hakuna mtu aliyepata kuweza kuwapitisha njia nyingine. Wao wanajua maskini kiongozi huyo atawaongoza hasa kufikia mahali pa Mungu palipowekwa. Naye anafanyaje jambo hilo? Kwa vifaa vyake vilivyotolewa na Mungu. Yeye amezinyosha antena zake, wakati wote, kama vile inavyotupasa kufanya, kumdaka Roho, antena zetu za kiroho.

¹⁷¹ Sasa, tunaona ya kwamba yeye ataruka hewani, huko juu sana hewani. Amezitoa antena zake. Yeye anajua aina ya chakula ambacho maskini mabata hawa wanapaswa kuwa wakila, wapate kumudu safari hii ya hewani. Kwa hiyo wakati anapoona kitu huko chini kabisa ardhini, utamwona akipaa juu, kisha anashuka. Kundi lote litashuka moja kwa moja chini, wapate tu yubile ya ulaji bora. Naye atatoa mlio, watapanda hewani tena, moja kwa moja kuelekea kusini. Hiyo ni kweli.

Kiongozi wa Mungu, kiongozi wa Mungu kwa ajili ya mabata. Hiyo ni kweli.

¹⁷² Ninataka kusema jambo lingine. Mwajua, kamwe hawajaweza kupata kisayansi, kupata njia nzuri zaidi kwa mtoto mchanga kupata anachotaka mbali na kukililia. Mnajua, hawawezi kumwelimisha apate kukoroma. Wala hawawezi kumwelimisha kuzungumza upesi hivyo. Lakini mnajua jinsi anavyokipata? Yeye huichukua tu njia ya Mungu iliyowekwa kwa ajili yake. Yeye hukililia, hupiga makelele, na kurusha mateke, na kulia kwa nguvu mpaka atakapokipata. Mnaona? Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo njia pekee, ni kukililia. Hawawezi kupata njia bora zaidi iliyowekwa kuliko njia ya Mungu iliyowekwa. Hiyo ni kweli. Tuliache tu. Na hayo mambo ya asili...

¹⁷³ Nilisimama, hapa sio muda mrefu uliopita, huko Ujerumani, nami nilikuwa nikizungumza na kundi kubwa la watu. Ndipo nikasema, "Kwani mna shida gani ninyi Wajerumani? Mnajua, nilikuwa nikishuka mtaani, ndipo mbwa akabweka, naye alibweka katika Kiingereza." Nikasema, "Mama alikuwa akijaribu kumtuliza mtoto wake mchanga huko kwenye gari, muda mfupi uliopita, naye alikuwa akilia, na alikuwa akilia katika Kiingereza." Nikasema, "Mbona tunavurugikiwa jinsi hii? Mnaona? Wanapitia njia ya Mungu iliyowekwa. Nasi tulitoka kwenye mnara wa Babeli, mnaona, wote tumevurugika." Hiyo ni kweli!

¹⁷⁴ Wanajua njia ya Mungu iliyowekwa ndiyo njia iliyo bora kuliko zote. Hawajui njia bora zaidi kwa mtoto mchanga kupata kile anachotaka kuliko kukililia. Kama vile Dk. Bosworth alivyozea kusema, "Mtoto mchanga aliaye kwa sauti kubwa zaidi hupata huduma bora zaidi." Hivyo karibu ndivyo ilivyo.

¹⁷⁵ Hilo linatumika kwa watoto wa Mungu. Ningeweza kuwalinganishia hilo. Mtu anasimama, juu, kasema, huku akitafuna chingamu yake vizuri sana, "Unajua, Baba, nipo hapa usiku wa leo. Kama unataka kunipa Roho Mtakatifu, vema. Nipo hapa. Lakini kama unataka kuniponya, nimeketi hapa. Lakini kama hutaki, mbona, vema. Ni mapenzi Yako, Bwana." Tayari ameandika mapenzi, hapa katika Biblia. "Haya ndiyo mapenzi Yako." Vema. Haya ni mapenzi Yake, papa *hapa*. "Na ikiwa unataka nimpate, nitampata. Lakini, hata hivyo, kama hutaki, mbona, ni sawa." Kamwe hutafika popote.

¹⁷⁶ Lakini acha huyo afike pale na kulia, kama Buddy Robinson. Alisimama katikati ya shamba la mahindi. Akamfunga nyumbu wake. Akasema, "Bwana, usiponipa Roho Mtakatifu, utakaporudi utakuta lundo la mifupa limelundikana papa hapa. Nitakaa hapa mpaka nitakapompata." Huko ni kumaanisha.

¹⁷⁷ Mungu sikuzote hupendekeza kwa watu Wake, watoto Wake waaminio, daima wapitie kwenye njia Yake iliyowekwa. Hilo

ndilo wazo la Mungu, kupendekeza kwa watoto Wake, njia Yake iliyowekwa. Lilia kile unachohitaji. Anakutaka ulie.

¹⁷⁸ Wakati Petro alipoanza kwenda, akitembea juu ya maji, alidhani alikuwa akiendelea vema. “Mnaona jinsi ninavyofanya makubwa?” Akaanza kuzama. Hakusema, “Vema, nadhani imeshindwa,” akizama mpaka chini, mapovu machache yakatokea, na hayo yalikuwa ndiyo tu yaliyokuwapo. Mnaona? La, la.

¹⁷⁹ Alilia, “Bwana, niokoe.” Amina. Nao huo mkono wa Milele ukanyoshwa ukamwinua tena. Kwa nini? Alilia kwa sauti.

¹⁸⁰ Hiyo ndiyo shida ya kanisa. Hatukai pale muda mrefu kutosha. Hatulii muda mrefu kutosha. Hatulishikilii. Kama mtoto mchanga anataka kitu fulani, yeye atarusha mateke na kulia kwa nguvu, ageuke mwekundu usoni. Tunahofu tutafutilia mbali (ni kitu gani, mnakiitaje?) wanja kutoka usoni mwetu, ama chochote kile, rangi hiyo. Unapata—unapata unachotaka kutoka kwa Mungu, utaiondoa, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo, haikubidi kuhofu kulihusu. Utazichafua nywele zako, bali hilo halileti tofauti yoyote. La. La, bwana.

¹⁸¹ Sasa, Mungu hatutarajii tuje Kwake na hotuba fulani ya kiakili. Ninakumbuka nilijaribu hilo wakati nilipojaribu kuokoka. Nilikuwa nikitaka kumwandikia barua na kuiweka mwituni, maana nilijua Yeye angepitia mwituni na kuniambia. Nimwambie ninajionea aibu, na mimi—mimi sikutaka kufanya hivyo. Ndipo nikaenda huko chini kuomba. Nikasema, “Sasa, hebu tuone. Niliona picha wakati mmoja, ambapo walishikilia mikono yao namna *hii*.” Nikasema, “Bw. Yesu, laiti ungalikuja hapa kwa dakika moja. Ninataka kuzungumza nawe kwa dakika moja tu. Ninasikiliza.” Hakuna mtu. Nikasema, “Nililifanya vibaya. Vema. Bw. Yesu, labda ninapaswa kulifanya *hivi*.” Nikasema, “Bw. Yesu, waweza kuja unisaidie? Mimi ni mwenye dhambi. Ninataka kuzungumza na Wewe kwa dakika moja.” Hakuna mtu aliyekuja. Nikaikunja mikono yangu. Nikasema, “Bw. Yesu, waweza kuja hapa? Nataka... Nasikia watu wakisema, ‘Mungu alisema nami.’” Nikasema, “Bw. Yesu, waweza kuja hapa? Ninataka kuzungumza na Wewe.”

¹⁸² Hakika, ndipo ibilisi akajitokeza jukwaani. Hivyo ndivyo afanyavyo. Huenda akakwambia, “Magoti yako yanauma. Hakuna haja ya kuomba, unaona. Wewe ngojea, ukaipate kesho usiku.” Yeye daima yuko karibu wakati wewe huko tayari. Ndipo akaniambia... Lakini daima, yale asemayo, jinufaishe na yale asemayo. Jinufaishe nao.

¹⁸³ Yeye akaniambia, “Wajua nini? Wewe tayari una umri wa miaka kumi na tisa, ama miaka ishirini.” Kasema, “Tayari una umri wa miaka ishirini. Umengojea muda mrefu kupita kiasi.”

¹⁸⁴ Nikasema, “Ee Mungu, nimengojea muda mrefu kupita kiasi. Bwana, hata ingawa Wewe hunisikii, nitakwambia, kwa

vyovyote vile. Daima nimetaka kufanya jambo hili.” Loo, ndugu, hilo lilimleta jukwaani. Mnaona? Ilikuwa ni nini? Nililia, rahisi tu. Kulia sana! “Bwana Yesu, Wewe uliliahidi, Bwana.” Yeye akaja jukwaani.

¹⁸⁵ Hiyo ndiyo njia ya kumleta jukwaani. Wewe ni mtoto mchanga tu. Lia, lia sana kwa ajili yake.

¹⁸⁶ Usijaribu kusema, vema, karibu kila kitu, kingine, na maombi makubwa yaliyoandikwa upate kuyakariri, kwa saa moja ama mbili. Hilo halifai chochote.

¹⁸⁷ Kama vile wasemavyo, “Hivi ulikariri sala?” La. Ni dhambi kukariri moja. Wewe omba moja. Usikariri moja. Omba moja. “Ikariri sala kwa ajili yangu.”

¹⁸⁸ Nikasema, “Usifanye hivyo kwa ajili yangu. Unaweza kuniombea, bali usikariri sala yoyote.” La, bwana. La. Ninii tu, niombee unapoomba. Vema.

¹⁸⁹ Lilia mahitaji yako. Hiyo ndiyo njia iliyowekwa na Mungu. Hivi Yesu hakulielezea wakati aliposema yule hakimu dhalimu, kwa mwanamke yule aliyelia usiku na mchana? Ni zaidi sana vipi Baba yenu wa Mbinguni atakavyowapa Roho wale wanaolia kwa ajili Yake, usiku na mchana? Tafuteni, endeleeni kutafuta. Bisheni, endeleeni kubisha. Endeleeni tu mpaka Yeye atakapofungua. Dumuni nalo. Lienii mpaka Neno lililoahidiwa limethibitishwa, ndipo mmelipata. Haiwabidi kufadhaika tena. Mkiona Biblia ililiahidi, basi dumuni pale pale na kulia mpaka mlipate.

¹⁹⁰ Kama mtoto mchanga akiona biskuti naye anaitaka, yeye hulua tu, na kulia, na kulia, na kushikilia, na kurusha mateke, na kulia kwa nguvu, na kupiga mayowe, na kugeuka mwekundu usoni. Mama yake akimpa biskuti, basi yote yamekwisha. Mnaona? Alipata kile alichona, kile alichotaka. Kama anataka kuiramba koni yako ya aiskrimu, ataendelea tu kufanya ghasia mpaka aipate. Mnaona?

¹⁹¹ Vema, hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Kama nikiona ahadi katika Biblia ambayo ni Neno la Mungu, basi nakaa hapo tu na kulia mpaka Mungu anipe hiyo. Naye angefanya hivyo, apate kukuondoa mikononi Mwake; unaona, hilo lingekuwa katika mambo ya kawaida. Lakini anakutaka ufanye hivyo. Anapenda wewe uombe. “Ombeni kwa wingi ili furaha yenu itimizwe.” Naam. Naam.

¹⁹² Lia mpaka Neno Lake lithibitishwe. Sasa, ewe rafiki, hebu tuangalie kwa dakika moja tu sasa. Lia mpaka Neno lithibitishwe.

¹⁹³ Shida yake ni kwamba, tunapata biskuti nasi tunafikiri hiyo tu ndiyo iliyoopo. Kuna meza nzima iliyojaa. Tunafikia ambapo tunaweza kunena kwa lugha, tunasema, “Loo, ndugu, jambo ndilo hilo.” Loo, la. Hilo silo. Hilo ni baadhi yake tu. Hiyo ni

kweli. “Loo, nilifurahi kutosha kupaza sauti.” Hiyo ni baadhi yake tena. Ila kuna mengi sana zaidi ya hiyo. Endelea tu kulia sana, mpaka . . .

¹⁹⁴ Hiyo ni njia ya Mungu iliyowekwa kwa ajili ya watu Wake. Njia ya Mungu iliyowekwa daima ni kuchukua Neno Lake na kulishikilia mpaka limethibitishwa kwako. Sasa, mnanifuata? Mungu, njia iliyowekwa, ishikilie ahadi mpaka imedhihirishwa kwako.

¹⁹⁵ Na, kumbukeni, nimewekewa kumbukumbu juu ya hili. Kwamba, ahadi yoyote ya Mungu katika Biblia, kama . . . Iko kwenye masharti sasa. Kwa sababu tu unaamini iko pale, hilo haliifanyi itimie.

¹⁹⁶ Hao Mafarisayo na Masadukayo walikuwa ni wa kidini tu pamoja na sakramenti hizo kadiri walivyoweza kuwa. Lakini Mungu alisema, “Zinanuka puani Mwangu.” Mnaona? Hakukuwapo na uaminifu wowote. Hakukuwako na kitu kwake kinachopaswa kuwa.

¹⁹⁷ Inakupasa kuja juu ya ahadi za kimsingi, na kisha juu ya msimamo wako wa kiakili kulihusu.

¹⁹⁸ Waangalieni wale makuhani mia nne siku hiyo, ama manabii, aliokuwa nao Ahabu kule. Wao walisema, “Ramothi-gileadi ni mali yetu. Yoshua, kwa Roho Mtakatifu, aliigawanya hii. Nao Waashuri wanayo.” Ndipo nabii mmoja akasema, “Sasa, angalieni hapa, hiyo kimsingi ni kweli.” Sasa, yeye alikuwa ni Mbaptisti halisi. Naye akasema, “Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni ahadi ya kimsingi, ahadi. Hiyo ardhi ni mali yetu.” Kwa hiyo akajitengenezea pembe mbili kubwa, na kusema, “Kwea uende huko, na uchukue pembe hizi ukawasukumie Waashuri mbali sana. Hiyo ni mali ya Israeli.” Hiyo ni kweli. Kimsingi, ilikuwa ni kweli.

¹⁹⁹ Lakini maskini Mikaya alisema nini? Yeye alisema, “Niliwaona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.” Mnaona?

²⁰⁰ Ahabu, yule mnafiki kule chini, akimwacha Yezabeli amwongoze kote, akifanya kila kitu. Neno halisi la Mungu likija kupitia nabii, lilikuwa limekilaani kitu hicho. Basi Mungu angewezaje kubariki kile nabii alikuwa amekilaani katika Jina la Bwana? Mnaona? Haiwezekani.

²⁰¹ Haijalishi sisi ni taifa la kidini jinsi gani, tuna msingi kiasi gani, kitu hiki kimepotoshwa na kupotoshwa. Kimekwisha.

²⁰² Haijalishi maisha yetu ya kimadhehebu ni makuu jinsi gani kanisani, tunayaamini, ni mazuri, vema, bali kitu hicho kimepotoka. Mungu tayari amewaweka kwenye rafu, nao hapo wamekaa. Wala hakuna kipande cha historia kwamba lolote liliwahi kuinuka tena. Kwa hiyo, ni kosa. Limekwisha, limefutuliwa mbali. Halifai kitu.

203 Neno Lake ndilo daima analotaka kuliona limethibitishwa. Litathibitishwa tu juu ya masharti fulani, hapo ni wakati mtakapotimiza masharti hayo. Mmewaona watu wanaoweza kulichukua Neno la Mungu nao wanalifanya tu kuwaishia. Halafu wengine wanarudi moja kwa moja na Neno lile lile nao hawawezi kufanya lolote Nalo. Ni kwa masharti. Hiyo ni kweli.

204 Angalieni hapa. Nitawaonyesheni mfano wa hilo katika Biblia. Israeli walikuwa njiani wakienda kwenye nchi ya ahadi. Hawa hapa Moabu wakaja, ambao walikuwa ni—walikuwa ni dini ile ile, hasa. Huyu alikuwa ni mtoto wa binti ya Lutu. Basi angalia wakati Balaamu aliposhuka, ilikuwa ni Mungu akizungumza naye. Aliweka madhabahu saba, kama tu Israeli walivyokuwa na madhabahu saba. Akaweka dhabihu saba safi, mafahali madhabahuni. Hao ndio Israeli waliokuwa nao hasa. Na jambo lingine, aliweka kondoo dume saba, ikinena kuhusu Masihi ajaye. Hao ndio hasa Israeli walikuwa nao. Kimsingi, wote wawili walikuwa sahihi, kimsingi. Ila ilikuwa juu ya masharti. Amina. Yeye alishindwa kuona ile ahadi halisi ya Mungu.

205 Hilo ndilo jambo lile lile lililokuwa katika kuja kwa Kristo. Hilo ndilo jambo lile lile limerudia siku hizi. Liko kwenye masharti. Kweli.

206 Ayubu. Mungu (akifanya nini?) akifanya njia iliyowekwa. Ayubu, nabii, alihitaji mfariji.

Sasa, sikilizeni kwa makini sasa. Wakati wangu umekwisha.

207 Ayubu alihitaji mfariji. Nao watu wakajaribu kumpa kitu hicho, nao wasingeweza kufanya hivyo. Sikuzote walimsukuma Ayubu kando. Bali Ayubu alirudi moja kwa moja. Alihitaji mfariji. Mungu akampa mfariji, hapo alipomwonyesha ono la Yesu Kristo. Naye akalia, “Najua Mkombozi wangu yu hai. Mkombozi wangu,” kunaye Mmoja tu, “na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi.” Sasa kumbukeni lile ono.

MLisema, “Mkombozi wangu.”

208 Yeye alimwonyesha Kristo. Kristo ni Neno. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Basi wakati Ayubu, akiwa ni nabii...

209 Sasa sikilizeni. Ayubu, akiwa ni nabii, Neno la Bwana humjia (nani?) nabii. Kweli kabisa. Hapo ndipo Neno linapokuja. Hivyo ndivyo unavyojua kama hao ni manabii ama sivyo. Wanadumu katika Neno. Neno hufunuliwa nabii. Naye Ayubu alikuwa ni nabii. Asingeweza kuona mwisho, bali wakati alipoliona Neno, akiwa ni nabii, yeye alisema, “Ninajua Mkombozi wangu yu hai,” baada ya kanisa kushindwa, baada ya kila kitu kingine kushindwa.

210 Hata mke wake mpendwa alikuwa amemkosea, na anamtaka aseme. . . “Mbona usitoke uende ukamkufuru Mungu, na ufe kifo, Ayubu?”

211 Akasema, “Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu. Bwana alitoa; Bwana ametwaa; Jina la Bwana libarikiwe.” Ndipo ngurumo zikaanza kunguruma, na radi kumulika. Roho akaja juu ya nabii, naye akaliona Neno. Ndipo akasema, “Najua Mkombozi wangu yu hai. Katika siku za mwisho atasimama juu ya nchi. Hata mabuu ya ngozi yakiuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu. Amina. Nitamwona mimi mwenyewe. Macho yangu yatamwona, na si mwingine. Hatukuleta chochote katika ulimwengu huu, na ni dhahiri hatutatoa chochote. Bwana alitoa; Bwana ametwaa; Jina la Bwana libarikiwe.” Ni Mfariji wa jinsi gani! Yeye aliomba apewe mshiriki wa kanisa; Mungu akampa ono. Aliomba askofu aje akamfariji, mzee wa jimbo; Mungu akampa huyo nabii ono. Hilo ndilo alilohitaji.

212 Israeli ilihitaji njia ya kutoka Misri. Walihitaji njia fulani, nguvu fulani za kijeshi ama kitu fulani, kuwakomboa kutoka kwenye mikono ya Wamisri. Mungu alimtoa nabii pamoja na Neno la asili lililothibitishwa. Musa! Hiyo ni kweli? Walitaka jeshi liinuke na kuwatoa huko, na kuwapiga Wamisri. Bali Mungu akawatumia Neno, nabii pamoja na Neno lililothibitishwa ambalo Mungu alikuwa amelinena hapo awali kwa Ibrahimu, akisema, “Uzao wako utakuwa mgeni katika nchi ya kigeni. Bali nitawazuru kwa mkono wenye nguvu,” Neno ambalo Mungu alikuwa amelinena. Walikuwa wakilia wapate mkombozi, naye Mungu akawatumia nabii akiwa na Neno. Mungu alikuwa na njia iliyowekwa ya kujua tofauti kati ya mwaminio na asiyeamini. Naye Mungu. . .

213 Sasa, baadhi yao walisema, “Vema, sasa, kama tauni ikishuka, tutaenda tu hospitalini. Kama tauni—kama tauni ikishuka, mnajua kile tutakachofanya? Tutaenda tumpate Dk. Jones. Yeye atajua jinsi ya kuishughulikia.” Hilo halikufanya kazi. Hata hivyo, wao walikuwa ni werevu. “Vema, tauni ikishuka, tutaingia tu chini ya ardhi, katika pango, na kufunga mlango vizuri.” Hilo halitafaa chochote hata kidogo. “Tutakaa nyumbani, na kuvaa barakoa juu ya uso wetu, na—na kupaka kiua viini fulani juu yake.” Halikufaa kitu hata kidogo.

214 Mungu alifanya njia iliyowekwa. Naam. Nayo ilikuwa ni (kitu gani?) damu. Mungu aliweka, rahisi kama ilivyoonekana, kuchukua damu ya mwanakondoo na kuinyunyizia mlangoni. Hata hivyo, Mungu alisema hiyo ilikuwa ndiyo njia Yake, na Yeye aliiheshimu. “Wote waliokuwa nje ya hiyo damu walikufa, wazaliwa wa kwanza.”

215 Nuhu alipohitaji njia iliyowekwa, kwa wokovu wa nyumba yake, Mungu alimfanya kuijenga safina. Huenda walijenga

mitumbwi ya dhahaka. Hivyo ndivyo watu wanavyowazia siku hizi. Lakini, mnaona, huu ulikuwa ni mtumbwi maalum. Labda walikuwa na mitumbwi wakati huo, kama waliyo nayo sasa, bali huu ulikuwa ni mtumbwi maalum. Ulikuwa ni... Nisikilizeni sasa. Ulikuwa ni mtumbwi ulioundwa na Mungu.

²¹⁶ Nalo kanisa siku hizi ni vile vile. Halina budi kuwa ni kanisa lililoundwa kwa Biblia. Ujuzi wangu sio kuwa mfuasi mzuri kuliko wote kanisani, bali ujuzi ulioundwa kwa Neno la Mungu. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Ujuzi uliojengwa na Mungu, ndicho kitu pekee kitakachonipeleka juu. Ndicho kitu pekee kitakachokupeleka juu.

²¹⁷ Chochote kitakachoinuka juu ya hilo, sijali ni wangapi, “Naja...” Kasema, “Tazama, mimi—mimi ni Mmethodisti mzuri, Mbaptisti, Mpresbiteri, au Mpentekoste.” Hilo halitamaanisha jambo moja kwa Mungu.

²¹⁸ Halina budi liwe limefunzwa na Mungu. Na huyo ni Roho Mtakatifu, kwa Neno. Naye Roho Mtakatifu kamwe hatafunza lolote ila Neno, kwa sababu Huyu ni Roho Mtakatifu. Wanadamu waliongozwa, loo, waliandika Biblia kwa Roho Mtakatifu, njia ya Mungu iliyowekwa.

²¹⁹ Sasa, Israeli ilihitaji ri—ridhaa. Naye Mungu akawapa, kisha akatenganisha mwaminio na asiyeamini. Ni jambo lile lile siku hizi, mwaminio na asiyeamini, wametenganishwa.

²²⁰ Musa, sina budi kuruka muhtasari mwingi sasa, lakini, Musa, mtumishi mwaminifu wa Mungu!

²²¹ Sasa sikilizeni, enyi watu wa zamani. Baadhi yenu kama mimi, wanaozidi katika miaka yao, sikilizeni.

²²² Musa alikuwa amemtumikia Mungu kwa uaminifu. Alikuwa amevumilia manung'uniko yao yote, na akina Dathan wote walioinuka na kusema, “Aisee, kuna watu wengine ambao ni manabii mbali na wewe. Wewe siwe changarawe pekee iliyo ufukoni.” Naye alijua alikuwa na Ujumbe wa Mungu kwa ajili yao. Waigaji waliinuka.

Musa alisema tu, “Mungu, nifanye nini?”

²²³ Na Yeye akasema, “Jitenge. Nitakimeza tu kitu hicho chote. Chukueni fimbo zenu, mwende mle ndani muone ni gani itakayochanua. Mnaona? Nitawaonyesha ni nani kuhani, ni nani nabii.”

²²⁴ Naye Musa alikuwa ameitumikia hiyo ofisi kwa uaminifu. Ndipo alipokuwa mzee, miaka mia moja na ishirini alikuwa ametembea kwa uaminifu pamoja na Mungu. Miaka hii yote arobaini nyikani, alistahimili kila namna ya mateso ya mataifa na ya watu, sikuzote. Ndipo basi ikafikia mahali pa kufa. Alihitaji mahali pa kufia. Mungu akamwandalia mahali juu ya Mwamba.

225 Ee Mungu, nijalie nife hapo, pia, juu ya Mwamba. Huo Mwamba ulikuwa ni Kristo, mwajua. Mungu aliandaa mahali pa Musa kufia. Hapo ndipo ninapotaka, mimi, ninapotaka kufia. Jalia nife katika Kristo.

226 Ndipo wakati alipokuwa amekufa, mwili wake umelala kule juu, alihitaji wabeba jeneza. Kwa hiyo Mungu akamwandalia wabeba jeneza, Malaika. Kwa nini? Hao Ndio pekee wangaliweza kumpeleka mahali alipokuwa akienda. Amina. Mungu alimwandalia wabeba jeneza. Hiyo ni kweli.

227 Ninamtegemea Roho Mtakatifu, juu ya Neno, ile ahadi. Sio kukupeleka kwenye mazishi mazuri makubwa. Walimfanyia hivyo yule tajiri, bali aliyainua macho yake kuzimu. Mnaona? Sio juu ya mazishi ya fahari. Hayaleti tofauti yoyote. Ninataka kuipitia njia ya Mungu iliyowekwa. “Hao walio katika Kristo Mungu atawaleta pamoja na Yeye atakapokuja.” Hiyo ndiyo ridhaa. Mungu alimwandalia nabii Wake mwaminifu mahali pa kufia.

228 Henoko, baada ya kutembea miaka mia tano pamoja na Mungu, basi Mungu alimwambia, “Henoko, haitakubidi kufa. Wataka kuja Nyumbani? Una shauku ya kwenda nyumbani, Henoko?”

Akasema, “Naam, Bwana. Nina shauku ya kwenda nyumbani.”

229 Akasema, “Umetembea katika nyumba hiyo ya wadudu huko chini muda mrefu kutosha?”

Akasema, “Naam.”

Kasema, “Vema, anza tu kutembea.”

230 Henoko alihitaji ngazi. Mungu akampa barabara kuu. Hiyo ilikuwa ndiyo njia ya Mungu kwa ajili yake. Alimpa barabara kuu, ya kwenda juu! Yeye hakuninii. . . Alienda tu moja kwa moja juu, namna *hiyo*. Haikumbidi kujikakamua, hata kidogo. Alikimbia tu moja kwa moja juu; naye Roho Mtakatifu, nyuma yake, akamwinua moja kwa moja juu. Alipanda moja kwa moja kwenye barabara kuu ya utakatifu, moja kwa moja akaingia katika Ufalme wa Mungu.

231 Eliya, akiisha kuwahukumu waliozikata nywele zao na kupaka rangi nyuso zao, kwa maisha yake yote, juu ya huyo Yezebeli, mama taifa, yeye na rais aliyejulikana sana wa wakati huo, walioweka mfano mbaya mbele za watu na kuwapotosha wote kabisa. Na—na, kwa kweli, yeye alidhani alikuwa ndiye pekee aliyekuwa akihubiri hayo. Alikipeleka tu kitu hicho kwa kila njia. Naye akafanya mengi sana, mpaka alikuwa anachoka, naye alitaka kwenda Nyumbani. Naye alijua Mungu alikuwa ni wa kutoka Juu. Alihitaji kamba ya kupanda juu, apate kufika Mbinguni, bali Mungu akamtumia gari pamoja na farasi wawili waliofungiwa kwake. Hiyo ni njia ya Mungu iliyowekwa ya

kumchukua. Huenda alikuwa akitafuta kamba, lakini Mungu akatuma gari. Hiyo ilikuwa ndiyo njia Yake. Yoshua. . .

²³² Ndipo mwishoni mwa safari, huo ulikuwa ndio mwisho wa Eliya. Huyo alikuwa ni Nuhu. Huo ulikuwa, wakati wote, ndio mwisho.

²³³ Sasa, Yoshua, wakati alipoufikia mwisho wa njia yake, kupitia nyikani, angalia, alihitaji daraja apate kuuvuka Yordani, kuingia kwenye nchi ya ahadi. Mungu. . . Yeye, yeye alihitaji daraja. Lakini njia ya Mungu iliyowekwa ilikuwa ni nguvu, si daraja. Yeye alituma nguvu, na Yeye akauzuilia ule mto. Ndipo akavuka juu ya nchi kavu. Hiyo ilikuwa ndiyo njia ya Mungu iliyowekwa, si daraja. Yeye alikuwa na Mhandisi bora zaidi. Kwa hiyo, Yeye alimtumia tu nguvu, akayasukuma maji nyuma mpaka akatembea juu ya nchi kavu.

²³⁴ Danieli, kwa ajili ya huduma ya Mungu, alitupwa katika tundu la simba. Alihitaji uzio, bali Mungu alimtumia Malaika. Ni tofauti jinsi gani! Hiyo ilikuwa ndiyo njia ya Mungu iliyowekwa. Alihitaji uzio, bali Mungu akampa Malaika. Lilikuwa ni ua bora jinsi gani! Yeye daima hukupa kilicho bora zaidi ya ulichoomba, sikuzote. Naam. Alihitaji uzio; Mungu akamtumia Malaika.

²³⁵ Wana wa Kiebrania, walihitaji maji, kuuzima ule moto. Bali Mungu akawatumia Mtu wa nne. Huyo tu ndiye waliyemhitaji. Aliifungua mikono yao, na kuzungumza nao. Wakatoka pasipo na harufu ya moto juu yao. Walihitaji maji; Yeye akamtuma Mtu wa nne.

²³⁶ Mamajusi huko Babeli, huko India, walijua kwamba jambo fulani linakaribia kutukia. Walijua Mfalme alikuwa amezaliwa, nao walihitaji dira. Mungu akawatumia nyota kuwaongoza kumfikia yule Mfalme. Mnaona? Waliendea njia ya Mungu iliyowekwa. Ninaweza tu kuwazia baadhi yao wakisema, "Aisee, Balthaza, wajua, wewe ni mtu mashuhuri. Hivi ulileta dira yako?"

Akasema, "La."

"Vema, utawezaje kufika kule?"

"Ninaiendea njia ya Mungu iliyowekwa." Hiyo ndiyo njia.

"Utafikaje kule?"

"Njia ya Mungu iliyowekwa."

"Ni kitu gani?"

²³⁷ "Hiyo Nyota, hiyo ndiyo. Hiyo ndiyo njia ya Mungu iliyowekwa kwa ajili yetu." Walihitaji dira, naye Mungu akawapa nyota.

²³⁸ Ulimwengu ulihitaji Mwokozi siku moja, naye Mungu akamtoa Mwana Wake. Wakati alipokuja, Yeye hakutambulikana. Hakutakiwa. Walisema walitaka Mwokozi.

Lakini wakati Mungu alipomtuma katika njia Yake... Waliomba wapewe mfalme; Mungu akawapa Mtoto mchanga. Walitaka mtu mwenye nguvu kuiondosha Rumi kwa kishindo. Mungu akawapa Mtoto mchanga, anayelia katika hori. Mnaona? Lakini ilikuwa ndiyo njia ya Mungu iliyowekwa. Sisi... Bali hawakuitaka jinsi Mungu alivyotaka kuituma. Wanaitaka jinsi walivyoitaka. Mnaona? Kwa hiyo, basi, wakaingia katika mchafuko kwa sababu hawakuikubali njia Yake. Kulikuwako na wengine walioikubali.

²³⁹ Hapa palikuwa ndipo mahali pa kuzaliwa kwa Kanisa, palikuwa ni Pentekoste, baada ya Yesu kuwaagiza “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Yeye alikuwa amewaambia la kufanya. Akawaambia wapande juu, mji wa Yerusalemu, na kungojea. Walihitaji mkataba. Walihitaji mkataba. Walitaka kuweka kanuni ya imani. Mungu akawapa Roho Mtakatifu. Loo! Walihitaji dhehebu, bali Mungu akawapa Roho. Ni tofauti jinsi gani, jinsi Mungu anavyolitenda! Roho Mtakatifu alikuwa ni njia ya Mungu iliyowekwa ya kuliongoza Kanisa, sio askofu. Roho Mtakatifu, hivyo ndivyo, huyo alikuwa ndiye mkataba wao. Na tangu siku hiyo, hata wa leo, amekuwa ndiye mkataba wa kila mtoto wa kweli aliyezaliwa mara ya pili: Roho Mtakatifu.

²⁴⁰ Sasa, baada ya miaka elfu mbili, enyi marafiki... Tunafunga. Sasa, baada ya miaka elfu mbili, mwanadamu amedhamiria kuwa na njia yake. Alijifanyia mkataba. Alijifanyia maadili yaliyobuniwa na mwanadamu. Naye alifanya nini? Kumetokea, kwa jambo hilo, kuanguka kukuu kutoka kwenye ile Kweli. Waliondoka kwenye... Watu hawajui la kufanya. Kanuni za imani, madhehebu, kila namna za itikadi, misisimko, na kila mtu anasema, “Biblia inasema *hivi*.” Watachukua sehemu *hii* Yake, bali hawatachukua sehemu *ile* Yake. Hawaufuati ule mkataba, kwa hiyo wanapoteza njia. Na baada ya miaka hii yote, wakati tuna madhehebu mbalimbali mia tisa na kitu ya Ukristo, na kila moja likilihukumu hilo lingine, na kusema, “*Hili* ni sahihi, na wao wamekosea; na *hili* ni sahihi, na *lile* ni la uongo,” na kadhalika. Nao maskini hao watu wamechanganyikiwa sana hawajui yaliyo kweli wala uongo.

²⁴¹ Tunahitaji nini? Tunahitaji kurudi kwenye njia, turudi kwenye mkataba. Tunahitaji nini? Tunahitaji ishara ya kweli ya Kimaandiko iliyo halisi, ya Kweli. Ukweli wa Injili uliothibitishwa ndio Kanisa linaohitaji kwa ajili ya njia hii ya wakati wa mwisho. Mungu aliahidi kuwapa ishara kwa ajili ya siku hii ya mwisho.

²⁴² Mnakumbuka wakati Yesu alipokuwa akizungumza na kusema, “Malkia wa kusini atasimama katika siku ya mwisho, atasimama na kukihukumu kizazi hiki kwamba kimekosa?” Alikuwa kutoka pande za mwisho wa dunia, aisikie hekima ya

Sulemani. Alikuwa na roho ya utambuzi. Jinsi alivyokuja kutoka mbali sana, aione roho hiyo ya utambuzi! Yeye akasema, “Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa.”

²⁴³ Alisema, pia, “Kama katika...kama nabii Yona. Yona, kama vile alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi, siku tatu mchana na usiku.” Naye akasema, “Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara.” Kama hii siyo hiyo ishara, ama kizazi hicho, sijui kiko wapi: kizazi dhaifu, kiovu, kinachohudhuria kanisa, cha zinaa. Wangeitafuta ishara, na Yeye alisema wataipata. “Kwa kuwa kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa katika moyo wa nchi.” Lakini kutakuwako na ufufuo, kama vile Yona alivyotoka katika tumbo la nyangumi.

²⁴⁴ Malaki, mlango wa 4, ilituahidi hilo katika siku za mwisho, ya kwamba, “Kutatokea Ujumbe ambao utaigeuza mioyo ya watoto iirudie Imani ya baba zao, ile Imani asili ya baba zao.” Waliliahidi. Yesu aliliahidi. Imani ya waaminio wa siku za mwisho itaona ishara asilia ya Masihi. Angalieni. Kama Yeye amefufuka kutoka kwa wafu, nazo kanuni za imani zimemtoa nje, miaka hii yote, na kuikana Kweli hiyo, basi jambo ambalo inatupasa kutafuta, katika siku za mwisho, ni kule kugeuka kuirudia ile—ile Imani ya asili, kuirudia ile Imani ya baba wa kipentekoste wa mwanzoni.

²⁴⁵ Nao waliuona ufufuo Wake. Na leo hii tunaona ufufuo Wake, ishara ya kufufuka Kwake. Yona, siku tatu mchana na usiku alikuwa katika tumbo la nyangumi, na siku ya tatu yeye akafufuka kutoka kwa nyangumi. Yeye alifufuka katika wafu, akiisha kuwa siku tatu tumboni mwake. Miaka elfu mbili Yeye amekuwa hayuko kanisani. Lakini Yeye aliahidi, kupitia Yoeli, “Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu. Lakini nitarudisha, asema Bwana, yote ambayo tunutu, na madumadu, na nzige, na kadhalika, walikula. Nitarudisha katika siku za mwisho.”

²⁴⁶ Nabii alisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Jua lile lile linaloangaza mashariki huangaza magharibi. Imekuwa ni siku, siku yenye giza. Wamejiunga, na kuweka kanuni za imani na kadhalika. Lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru: jua lile lile, matokeo yale yale, ishara zile zile, maajabu yale yale, wakati wa jioni.

²⁴⁷ Yeye alijithibitishaje Mwenyewe kwamba ni Masihi? Sasa, swali ni kwamba, baada ya miaka elfu mbili ya kulishambulia, hivi Yeye angali ni Masihi? Vema, kile alichokuwa wakati huo, Waebrania 13:8 ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Alichokuwa wakati huo, Yeye hana budi kuwa vivyo hivyo leo hii. Yeye alijithibitishaje Mwenyewe kuwa ni Masihi? Kulingana

na Neno la Mungu. “Kwa kuwa Mungu alikuwa amesema,” kupitia Musa, “Bwana Mungu wenu atamwinua nabii kama nilivyo mimi.”

²⁴⁸ Hiyo ndiyo sababu yule mwanamke kisimani, alipomwambia dhambi zake, “Mbona,” yeye alisema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Tunajua ajapo Masihi Yeye atatwambia mambo haya.”

Yeye akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

²⁴⁹ Akakimbia upesi na kuwaambia watu mjini. “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia yale niliyofanya. Haimkini kuwa huyu ndiye hasa Masihi?” Na hao watu wakaamini, kwa sababu walikuwa wakiitazamia ishara hiyo ya Kimasihi, miaka mia nne bila nabii.

²⁵⁰ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu,” wakati Mungu alipojifunua Mwenyewe katika mwili wa nyama, akala nya—nyama ya ndama, kanywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, na kuketi pale mbele yao. Mungu, Yehova, Yeye akidhihirishwa katika mwili, huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, na kusema yale Sara alikuwa akizungumzia hemani.

²⁵¹ “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Neno la Mungu lililothibitishwa ndilo ishara ya siku hii tunayoishi. Itakuwa Nuru. Na Yeye aliahidi, kupitia Malaki 4, kupitia mahali pengi pa Biblia, ya kwamba watu wa wakati wa mwisho wangeona dhihirisho lile lile waliloliona, maana Yeye hawezi akaibadilisha ishara hiyo. Ameahidi jambo hilo.

²⁵² Sasa, tulimsikia akinena kwa lugha pale Kalvari. Tumemwona akiyafanya mambo yote aliyofanya. Tuliliona Kanisa la kimitume kule nyuma kwenye mwanzo, jinsi ambavyo Kanisa la kimitume, hatua walizochukua. Tunaliona likirudi moja kwa moja Kanisani tena hapa katika siku za mwisho. Ni kitu gani? Ni Mungu, akithibitisha, kama tu alivyomfanyia Musa, kama alivyofanya kupitia nyakati. Yeye ameweka njia tusije tukadanganywa, ili tuweze kujua. Yesu alisema, katika Yohana 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, ishara nizifanyazo mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Hiyo itakuwa ndiyo. Sasa, kama Yeye alikufa na Yeye amekufa, basi kazi hizo zilikoma. Lakini kama Yeye yu hai tena, basi kazi Zake zinaendelea kama zilivyokuwa, kwa kuwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo?

²⁵³ Sikilizeni. Hebu niseme jambo hili: Yesu alithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, kwa ishara za Biblia za Masihi. Yeye alilithibitisha. Alikuwa hivyo. Sasa, Mungu na anijalie kuthibitisha sasa ya kwamba Yeye angali ni yeye yule. Mnaamini hilo? Yeye alilithibitisha. Alikuwa hivyo. Yeye alithibitisha alikuwa. Nijalie, kwa neema ya Mungu, kuthibitisha ndivyo Yeye alivyo. Yeye alithibitisha alikuwa hivyo. Hebu tuthibitishe kwamba Yeye ndiye. Hivyo hasa ndivyo

Yeye alivyoahidi. Hayo ndiyo aliyosema. Hivyo ndivyo Yeye alivyolielezea. “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

254 Ni kitu gani? Njia ya Mungu iliyowekwa, njia ya ufufuo. Kitu ambacho humleta mtu kutoka kwa ujinga wake, kikamwingiza katika Nuru ya Injili; kinamleta kutoka kwenye ubongo wa akili, kama mfumo mkubwa wa mashine, na kuunyenyekeza moyo wake mbele za Mungu.

255 “Vema,” mnasema, “mtu huyo ni mwerevu sana, Ndugu Branham. Alikuwa na digrii nne. Ana Shahada ya Sanaa. Yeye ana *haya yote*.” Sijali ana nini. Itambidi kusahau kila kitu alichojifunza, apate kumjua Kristo. Hiyo ni kweli. Itambidi kujinyenyekeza na kuondokea chochote ulimwengu ulichomfanyia.

256 Nawe unamjua Kristo kwa unyenyekevu, ukimwamini Yeye. Ni wakati wa jioni. Nilisema nini hapa, hapo mwanzo? Ni kitu gani nilichonena hapa? *Kuikubali Njia ya Mungu Iliyowekwa Katika Wakati Wa Mwisho*. Kila mmoja wa watu hawa, kila wakati kote kupitia Biblia, kupitia maumbile, tunaona...

257 Sasa, Mungu hachukui mti leo, na kuufanya kitu kingine, na halafu kesho aufanye kitu kingine. La. Yeye hufanya, leo—leo, utomvu unashuka chini, kesho unarudia njia nyingine, na wakati huo mwingine Yeye anawafanya kuuvuta huo utomvu juu? La.

258 Yeye hudumu moja kwa moja kwenye mkondo. Na kila mmoja wa watu hawa tumezungumza habari zao, kote katika Biblia, Mungu alikaa moja kwa moja kwenye njia Yake pamoja nao, kwa Neno Lake kabisa. Hakuna hata mmoja wao asiye kuwa kwenye Neno Lake hasa, kote katika Biblia, kwenye Neno Lake hasa.

259 Ndipo unaposema, “Vema, mimi niko kwenye Neno Lake kabisa,” ndipo Yeye anathibitisha hilo kwamba ni Kweli.

260 Sasa Yeye angali kwenye njia, usiku wa leo, kama tu tutaamini. Mtafanya hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

261 Na tuinamishe kichwa chetu. Sasa, kwa uchaji tu uwezavyo kuwa, kwa dakika moja.

262 Njia ya Mungu iliyowekwa, ili aweze kuwaleta waaminio kwenye Imani ya Kunyakuliwa. Njia ya Mungu, njia Yake aliyoiweka, kuwaleta waaminio kwenye Imani ya Kunyakuliwa.

263 Kabla sijafanya wito wa madhabahuni, ningetaka kusema jambo hili. Ninajisikia kuongozwa kufanya jambo hili. Kunao watu wagonjwa katika nyumba hii? Inua mkono wako.

264 Nitawaomba tafadhalini mwe watulivu tu, mketi kimya, kwa dakika moja zaidi. Sasa, tutakuwa tumetoka katika dakika zingine tano, kama mtakuwa tu na kicho kabisa.

²⁶⁵ Sasa, mnaona, ninyi, wakati unapokatiza, unamkatiza mtu fulani.

²⁶⁶ Nimeweka kitu hiki chote chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu. Lazima niwe nao, kusudi nifanye hivi. Mungu alitoa ahadi. Haikuwa ni mimi. Ilikuwa ni Yeye aliyeifanya hiyo ahadi.

²⁶⁷ Sasa, nijuavyo mimi, kunao watu hapa niwajuao. Kunao wengine nisiowajua. Kwa kweli ninaweza kuona yapata, nadhani, yapata watu wanne niwajuao. Na mmoja wao ni Ndugu Williams hapa, na Ndugu Rose. Ninawafahamu. Na Mama Sharrit ameketi huko mlangoni. Mimi, hakika, ninamfahamu. Huyu hapa Dada Williams ameketi hapa. Ninamfahamu.

²⁶⁸ Na mama huyu anayeketi papa hapa, yapata safu mbili mbele yangu hapa, anafanya kazi kwenye duka la bidhaa kavu, naye ni rafiki wa familia. Sijui jina lake, bali ninaamini yeye ni mfuasi wa kanisa la Ndugu Outlaw hapa juu. Nafikiri hiyo ni kweli.

²⁶⁹ Halafu ninamwona Ndugu Dauch na Dada Dauch, kutoka Ohio, wameketi hapa. Nilimsikia Ndugu Sothmann, huko nyuma kabisa mahali fulani, akisema, “amina,” muda mfupi uliopita. Ninaangalia. Hao ni karibu wote ninaowaona na kuwafahamu humu ndani.

²⁷⁰ Ni wangapi wenu walio wagonjwa, nanyi mnajua kwamba siwajui, inueni mikono yenu, ambao wanajua sijui lolote kuwahusu, inua mkono wako. Vema. Ninyi iweni tu na imani sasa na muamini.

²⁷¹ Sasa, kama nimewaambia Kweli, Mungu anawajibika kulithibitisha Neno hilo kwamba ni Kweli. Hiyo ni kweli? Ni kweli. Sasa, hiyo itakuwa ndiyo njia iliyowekwa basi, kulingana na yale niliyosema usiku wa leo. Hiyo ndiyo njia ya Mungu iliyowekwa ya kuwaambia, “*Hii* ni Kweli.”

²⁷² Kwa sababu, mtu yeyote anajua ya kwamba haiwezekani kabisa. Ingekuwa ni mwujiza ambao sayansi haiwezi kueleza. Huwezi kueleza mwujiza. Hauwezeki. Na ikiwa Mungu atanena hapa ndani, usiku wa leo, kwa mtu mmoja ambaye angejua ya kwamba nilikuwa mgeni kwao, na kuwaambia yale waliyokuwa wamefanya, ama yale ambayo hawakupaswa kufanya, ama yale watakayofanya, ama yale wanayopaswa kufanya, ama kitu fulani, kama tu vile Yesu alivyofanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani. Yeye alijitambulisha Mwenyewe kwa umma kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Ni wangapi wanaojua hayo, semeni “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi, kanisa linaamini hilo. Hiyo ndiyo njia pekee. Hao watu, wakati Yeye alipofanya hivyo, wao . . .

²⁷³ Yule mwanamke aligusa upindo wa vazi Lake. Akageuka, kasema, “Ni nani aliyenigusa?” Kimwili, Yeye hakumhisi, bali imani yake ndiyo iliyomgusa.

²⁷⁴ Sasa, unaweza kuwa na imani ya namna hiyo kama tu utaomba na kusema, “Bwana Yesu, ondoa kila shaka kutoka kwangu. Ondolea mbali mashaka yangu, na unijalie kuamini hili. Nina haja kubwa mno. Nami naja, usiku wa leo, kwa kuwa Biblia inasema ya kwamba Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.”

²⁷⁵ Hivi mlijua, ishara hii, mwujiza huu, haujafanywa katika historia tangu kifo cha mtume wa mwisho? Hiyo ni kweli. Ndio kwanza nipitie kwenye—kwenye... vitabu vyote vya historia nijuavyo mimi, *Babeli* kilichoandikwa na Hislop. Nimepitia *Kitabu cha Wafia Imani cha Foxe*. Nimepitia Wazee waliotangulia Nikea, Baraza la Nikea, na wa baada ya Nikea. Nimevipitia vitabu hivyo vyote. Hata mahali pamoja sijalion, katika historia ya Martin Luther, John Wesley, ule uamsho wa kwanza, uamsho wa Kiwelshi. Wamekuwa wakilia, wakipaza sauti, wakimsifu Mungu, hatimaye wakafikia kwenye kunena kwa lugha. Halafu basi hii ilipaswa kuwa ndiyo ishara ya mwisho. Hilo lilikuwa ndilo jambo la mwisho Sodoma uliloona kabla haujateketezwa.

²⁷⁶ Pia kumbukeni, Yeye hakulifunua kwa Sodoma. Alilifunua kwa Ibrahimu, aliyechaguliwa na kuteuliwa. Nayo karama hii haiyaandei makanisa ya kilimwengu huku nje, kama ukiangalia. Inaliendea Kanisa teule. Hao ndio wale wanaofaidika nayo. Ndio watakaoipokea.

²⁷⁷ Kama ingefanyika huko nje, wangesema jambo lile lile walilosema wakati Yeye alipoifanya, “Yeye ni Beelizebuli, mpiga ramli.” Na mtu yeyote anayejua kuhusu mpiga ramli, anajua hilo ni—hilo ni jambo la kiwazimu hata kulitamka. Wao hawajui kanuni ya kwanza ya telepathia wala ya upiga ramli. Hiyo ni kazi ya ibilisi, akijaribu kuiga kazi ya Mungu.

²⁷⁸ Mungu humwonyesha nabii; ibilisi ana kijumbe. Hao wawili wanafanana sana. Yesu alisema karibu ingewapumbaza walio Wateule, kama yamkini. Ni kweli. Tuna ninii mwingi—uigaji mwingi sana. Akasema, “Kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Musa, vivyo hivyo na watu hawa wenye akili potovu, waliokataliwa kwa mambo ya Kweli. Lakini upumbavu wao utajulikana.”

²⁷⁹ Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninawaweka wasikilizaji hawa chini ya mamlaka yangu, bali kwa ajili ya Roho Mtakatifu, kwa Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁸⁰ Ninawasihi, kama waaminio, msisogee. Ketini kimya. Nanyi muamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ya kwamba nipo hapa kuzitambulisha kazi Zake na njia Zake.

²⁸¹ Nimekuwa nikisita sana kwenye mambo haya, miaka hii kumi na mitano, kumi na sita ambayo nimekuwa hudumani.

Lakini kuna saa inayokuja sasa ambapo jambo fulani linakaribia kutukia. Huu Ujumbe utaenda kwa taifa lingine, watu wengine. Lakini wakati tukiwa Mbele ya Utu Wake Mtakatifu... Kanisa katika Marekani, ninaamini, karibu limeitwa lote. Limekwisha, limeoshwa, liko tayari, Kanisa halisi. Unafiki ungali upo. Bali Kanisa la kweli lilikuwa ni Kanisa la kweli, tangu mwanzo, limezaliwa mara ya pili, likachaguliwa tangu zamani kwa wito wa Mungu.

²⁸² Kama unaamini kwa moyo wako wote, ninakusihi uombe na kusema, “Bwana Yesu,” moyoni mwako, “jalia niliguse vazi Lako. Nami nitajua je ya kwamba Wewe ungali ni Kuhani Mkuu yeye yule? Zungumza nami kupitia midomo ya Ndugu Branham. Na kama ameniambia Ukweli, ambao, ninaamini ameniambia.”

²⁸³ Hakikisha kutaja hilo katika maombi yako, maana Yeye aliniambia, “Ukiwafanya watu kukuamini.” Hiyo ndiyo pekee... wewe... Yeye asingeweza kutenda kazi nyingi kubwa, kwa sababu wao hawakumwamini. Msiniamini mimi kama kwamba ni Yeye, bali aminini kwamba Yeye alinituma. Nami nipo hapa kumdhihirisha Yeye. Yeye alithibitisha kwamba alikuwa. Mungu na anijalie kuthibitisha kwamba Yeye amefufuka kutoka kwa wafu, Masihi, yeye yule jana, leo, na hata milele.

²⁸⁴ Sasa iweni tu katika maombi. Ninaangalia na kungojea. Ombeni tu. Basi ikiwa Bwana atatujalia, na atathibitisha kwenu ya kwamba hii ndiyo ishara ya wakati wa mwisho, mtatembea katika hiyo Nuru? Mtamwamini, mwe na imani Kwake? Yeye hana upendeleo. Iweni tu na imani, kote, kila mahali. Sasa, wakati vichwa vyenu vimeinamishwa, ninamshukuru Bwana.

²⁸⁵ Hii hapa ile Nuru mnayoiona katika ile picha. Yeye yuko papa hapa ndani ya chumba hiki sasa. Nami ninaiona Hiyo moja kwa moja karibu na mwanamke anayeketi mkono wangu wa kulia. Yeye anamwombea mwanawe aliye katika shida. Usitie shaka. Kuwa na imani.

²⁸⁶ Kwenye mkono wangu wa kushoto kuna mwanamke, naye anahofia. Anahofia kwamba ana kansa. Ameshtuka sana kuhusu hiyo. Ninatumaini hataikosa. Mwanamke huyo amejaribu, kwa muda mrefu, kupenya aingie ndani. Anaogopa. Hatoki hapa. Anatoka kwenye mji mwingine. Nao mji huo ni mji mdogo kuliko huu, ingawa uko kusini kutoka hapa. Upo kando ya mlima. Ni Tucson. Jina la mama huyo ni Bibi Bach. Unaamini? Utaukubali uponyaji wako? Vema. Usitishwe nao tena. Imani yako inakuponya.

²⁸⁷ Mama mmoja jina lake Bibi Hushey. Usisahau. Mungu anaweza kuthibitisha kwamba mwana huyo hana hatia, kama utaamini kwa moyo wako wote. Usitie shaka. Kuwa na imani. Amini.

²⁸⁸ Mama anayeketi hapa kando mkono wangu wa kulia, anaugua ugonjwa wa moyo. Jina lake ni Bibi Cloud. Kama utaamini kwa moyo wako wote, ukubali uponyaji wako, Mwenyezi Mungu atakuponya. Utaamini? Vema. Wewe amini kwa moyo wako wote.

²⁸⁹ Mama mmoja hapa nyuma kabisa mkono wangu wa kulia, kwenye safu ya mkono wa kulia, aliyevaa gauni jeusi. Bibi Yates, amini kwa moyo wako wote, nao ugonjwa wako wa mgongo utakuacha. Loo, jamani!

²⁹⁰ Mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnamwamini Yeye? [“Amina.”] Ni Yeye yule jana, leo na hata milele? [“Amina.”] Sasa, kama akilithibitisha hilo, nanyi mwone kwamba ni kweli, nao watu hao watashuhudia sijawahi kuwaona maishani mwangu.

²⁹¹ Lakini, angalieni, sasa, kama mtaliadini neno langu kwa yale ninayosema, kama mtaamini kwa moyo wenu wote na kuweka mikono yenu mmoja juu ya mwingine, mtaonywa kama mtaamini tu kwa moyo wenu wote. Ni ishara ya wakati wa mwisho.

²⁹² Sasa ninyi wekeni mikono yenu mmoja juu ya mwingine, ninyi mnaoenda kuombea. Kama wewe ni mwenye dhambi, kiri dhambi zako. Kama wewe umerudi nyuma, kiri kwamba umekosea. Ukiwa mgonjwa, kiri kwamba unataka kuponywa, na useme, “Ninakuamini Wewe, Mungu.”

²⁹³ Sasa, Biblia kamwe haikusema, “Maombi tu ya William Branham ndiyo yatakayofanikisha hili.” Bali Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mnaamini hilo?

²⁹⁴ Sasa, ni mara ngapi, ni muda gani nimekuwa nanyi, Phoenix? Hii ni kama miaka kumi na saba, nimekuwa nikija hapa. Mmewahi kuliona likithibitishwa kwamba limekosea wakati mmoja? Je, sikuzote limekuwa tu vile hasa Roho Mtakatifu alivyolinena? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kupitia maelfu mara maelfu, na kupitia mara nyingi mno; ni mara ngapi kote ulimwenguni, mataifa yote, na jamii, lugha, na watu; ni Yesu Kristo, sio ndugu yenu. Nami ninawanukulia Neno Lake. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

²⁹⁵ Sasa wekeni mikono yenu juu ya mtu fulani na kuwaombea. Usininii... Usijiombee mwenyewe sasa, kwa sababu wao wanakuombea. Wewe waombee. Na sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu katika Uwepo adhimu wa Yesu Kristo, Yule anayejithibitisha Mwenyewe kuwa miongoni mwetu. Sasa, Yeye ni Mungu wenu, kama Yeye alivyo Mungu wangu. Sasa wewe omba jinsi unavyoomba kanisani mwako. Mwombee mtu huyo aliyekuwekea mikono yao juu yako. Wewe waombee pia, na umwamini Mungu.

296 Kiri dhambi zako, sema, “Nimekosea, Bwana. Nimekuwa mwenye kushuku; sitakuwa hivyo tena. Ninaamini sasa hivi ya kwamba Wewe utaniponya.”

297 “Mponye mtu huyu, Bwana. Mponye mwanamke huyu. Mponye mwanamume huyu. Mponye mwanamke huyu. Mponye huyu mtoto mchanga. Mponye huyu msichana mdogo, huyu mvulana mdogo.”

298 Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, tunawezaje kuketi hapa, Bwana? Hii inapaswa kuleta Imani ya Kunyakuliwa, nguvu za Mungu ambazo zingeneza kwenye kusanyiko hili lote, Bwana, liingie kwenye maeneo ya juu zaidi, na kwenye utukufu wa Mungu.

299 Jalia ibilisi, ambaye amewafunga watu hawa, awaachilie; juu ya a—ahadi ya Mungu ninayoamini, juu ya Biblia ninayofundisha, juu ya Mungu Yule anayethibitisha ya kwamba ni Biblia, anayethibitisha kwamba Yeye ndiye Mungu wa Biblia. Baada ya miaka elfu mbili, Yeye angali anaishi miongoni mwetu usiku wa leo, amefufuka kutoka kwa wafu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Juu ya msingi wa Damu Yake iliyomwagika, na Utu Wake ulio hai, Uwepo, baada ya miaka elfu mbili, ninampa ibilisi changamoto, pamoja na roho yake yote dhaifu ya maradhi na magonjwa, awaachilie watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo. Toka ndani yao, wapate kuwa huru. Mwachilie mwenye dhambi huyo. Mwachilie huyo aliyerudi nyuma. Mwachilie huyo mwanamume mgonjwa ama mwanamke. Ninaudai uponyaji wao, wokovu wao, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Waache, ewe roho wa kuchukiza, mwovu, mchafu wa kutokuamini na mashaka. Ondoka kwenye kanisa hili, kutoka kwenye kundi hili la watu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

300 Ninaamini. Naamini ya kwamba maombi ya imani yameombwa. Ninawatakeni mfanye jambo fulani sasa. Papo hapo mlipo, shindilia nguzo niani mwako, “Papa hapa kwenye kiti hiki, usiku wa leo, niliposimama na kulisikia Neno, nikamwona Mungu akilithibitisha Neno Lake, kuthibitisha kwamba ni kweli, maombi ya imani yameombwa kwa ajili yangu. Iwapo shetani kamwe atajaribu kuniambia tena mimi ni mgonjwa, ama lolote baya, nitamrudisha moja kwa moja kwenye nguzo hii. Sasa hivi nimeombewa maombi ya imani, nami nimeokolewa kutokana na maradhi yangu. Nimeokolewa na dhambi zangu. Mimi ni mtoto wa Mungu, nami sitaupatia nafasi uongo wa ibilisi tena. Mimi ni mtumishi huru wa Mungu.” Amina. Mtafanya hivyo? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Inua mkono wako na kusema, “Ninaliamini.” [“Ninaliamini.”] Amina. Amina.

301 Kwangu mimi, hilo linatosha. Kazi imemalizika. Yote yamekwisha. Mungu alisema hivyo, na hilo linalithibitisha. Anawezaje kufanya jambo lingine lolote ila kulithibitisha

Neno Lake? Kama atalithibitisha kwangu, Yeye anaweza kulithibitisha kwako. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

³⁰² Na tusimame kwa miguu yetu na kumsifu, basi, tumpe Yeye sifa zote na utukufu. Amina. Vema. Utukufu kwa Mungu!

³⁰³ Asante, Bwana Yesu. Tunakupenda. Tunakusifu. Tunayakubali mambo haya. Tunaamini ya kwamba Wewe unatutendea hivyo sasa. Wewe ni Mwokozi wetu. Wewe ni Mponya wetu, nasi tunakupenda Wewe kwa ajili yake. Jina la Bwana na libarikiwe, milele. Wapokee watu hawa, Bwana, na uwajalie wawe watumishi Wako tangu sasa na kuendelea, kwa Jina la Yesu.

Mungu awabariki.



KUIKUBALI NJIA YA MUNGU
ILIIYOWEKWA KATIKA WAKATI WA MWISHO SWA63-0115
(Accepting God's Provided Way At The End Time)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumanne jioni, tarehe 15 Januari, 1963, kwenye Kanisa la Mataifa Yote huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org